# Roho Mtakatifu Alitolewa Kwa Kusudi Gani?

Mnaona, Ndugu Neville anaamini katika kuwekelea mikono.

Ninaona nina baadhi ya maswali. Sasa, nitachukua haya kesho usiku, maana sina wakati wa kuyachunguza usiku huu kwa ajili yenu, labda kwenye Ujumbe wa jana usiku. Naam, kama mtu ye yote ana swali juu ya Ujumbe wo wote, yawekeni tu usiku mmoja, nami ninaweza kuyachukua usiku ufuatao.

2 Sasa, kesho usiku ningetaka kupata, ama kuwa na, hasa, baadhi ya wahudumu, ikiwezikana; la sivyo, baadhi ya wanaume ama wanawake wazuri waliokomaa ambao tunaweza kuwapigia simu wakati wa haja, ili kwamba endapo . . .

Kesho usiku tutaanza, baada ya Ujumbe, kuwekelea mikono, na, kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Halafu, kutakuwa na . . . Utakuwa na majaliwa yako ya kukaa papa hapa ukitaka, kwenye likizo yote, kama itachukua muda mrefu namna hiyo kufa. Halafu—halafu, la sivyo, kama ukitaka kurudi nyumbani kwenu, mbona, tungefurahi, kama ungeingia mahali ambapo uta-. . . Hujui tu mahali utakapokwenda . . .

Tunataka kupata baadhi ya wahudumu, idadi yao, kama wao ni wageni; namba yao, mahali wanapokaa, mahali ambapo tungeweza kuwapata mara moja; kisha tumpeleke mmoja kwenye nyumba moja, na mmoja katika nyingine, mwingine katika nyingine, ili waweze kuwapa mafunzo, ninyi ambao mtatafuta baraka hii kuu tunayonena habari zake, ubatizo wa Roho Mtakatifu.

3 Jana usiku tulikuwa tukizungumzia, "kwamba Yeye alikuwa ni nini." *Roho Mtakatifu Alikuwa Nini*? Nasi tukakuta kwamba Yeye ni karibu kila kitu, ambacho Mungu alituahidi. A-ha. Katika Yeye tulipata kile tu Kanisa la Mungu lingehitaji. Tulipata kwamba Yeye ni muhuri, Mfariji, raha, furaha, na amani, na ufufuo. Na yote yale Mungu aliliahidi Kanisa Lake, yako katika Roho Mtakatifu.

4 Basi sasa, usiku wa leo, tunataka kuhubiri juu ya, ama kuzungumza juu ya, kufundisha juu ya . . . Nina kama makaratasi matatu manne ya vifungu hapa, ama Maandiko, juu Yake, ambamo . . . Jana usiku niliacha kamusi yangu ya Crudence hapa, nami sikuipata. Nami ilinilazimu kuyachunguza Maandiko vizuri nilivyoweza leo. Sasa, na kesho . . . Usiku wa leo tunafundisha juu ya: *Kusudi la Mungu la Kumtuma Roho*

*Mtakatifu Lilikuwa ni Nini*? Yeye ni wa nini? Kama ni kitu kikubwa namna hiyo, basi kwa nini Mungu akamtuma?

5 Halafu, kesho usiku tunataka kuzungumza juu ya: *Je! Yeye ni kwa Ajili Yako*? na *Je! Unampataje*? na *Unajuaje Unapompata*?

Halafu, baada ya kupitia katika jambo hilo, kwa Maandiko, kulieleza kwa Maandiko, tukitumia Maandiko kwa mambo yote, basi wale wanaomtafuta Roho Mtakatifu watakuja mbele wakati huo. Ndipo basi, natumainia ufufuo umewaka moto tangu wakati huo, tupate kuendelea basi na Roho Mtakatifu.

6 Sasa, kwa kuwa kesho usiku huenda wengi wakakaa kwa muda mrefu mle vyumbani kanisani, naona kama tungewapata wahudumu wengi na hao watu ambao wana ujuzi katika kuwaongoza watu kumpokea Roho Mtakatifu, kuwatia moyo, kwenda nyumbani pamoja na mwa—mwanamke na mumewe, ama—ama pamoja na mtu anayemtafuta Roho Mtakatifu, waliofunzwa vizuri juu ya jambo la kufanya.

Kama tu utampa mchungaji namba yako ya simu ama anwani, usiku huu ama kesho usiku. Mpe tu Ndugu Neville, ndipo jambo hilo litatupunguzia kazi ya kukutana kwa ajili ya mkutano. Toa tu namba yako ya simu mahali tunapoweza kukufikia. Halafu useme, "Nitakuwa tayari, na iwapo... mnataka kuniweka katika nyumba fulani." Kama ni mwa—mwanamke peke yake, basi tungeweza kumtuma mwanamke, mwaona, kwa mwanamke huyu. Halafu basi, kama ni katika nyumba ambamo kuna mwanamume na mkewe, mbona, tungeweza kumtuma mhudumu.

Nasi tungefurahi kama mkisaidiana, kwa maana ninajua, kila mmoja wenu, mnataka jambo hili, hili ni muhimu sana. Tena kumbukeni, "Yeye anayemwokoa mtu kutoka katika kosa lake, ameficha wingi wa dhambi." Mnaona? Naye Bibi-arusi wa Kristo anaona njaa na kiu. Yeye ana utungu, kuwazaa watoto wa Mungu.

7 Basi sasa, usiku wa leo, kabla ya kuyasoma Maandiko, na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu wa maombi. Na kabla tu hatujaomba, ninyi mlioinamisha vichwa vyenu, mngekuwa na haja? Inueni tu mikono na kusema, "Mungu, nainua mikono yangu kwa kicho. Nina haja. Nami naomba ya kwamba Wewe utanisaidia, Ee Bwana." Mungu ambariki kila mmoja wenu. Yeye anaiona mikono yenu. Malaika wameandika haja zenu.

8 Tena, Baba wa Mbinguni, sasa tunakuja, tukikukaribia Wewe tena katika maombi. Jambo ambalo, hapana shaka kwamba ombi tayari limetolewa miongoni mwa wana wa Mungu usiku wa leo, katika mahali hapa padogo, na kwamba nyimbo zimeimbwa, nasi tumeinua mioyo katika furaha ya shangwe katika kumsifu Mungu.

9 Daudi alisema angekuja katika kusanyiko la watakatifu kufanya dua yake ijulikane. Basi usiku huu, kumekuwa na mikono mingi. Labda, huenda ikawa, ningesema, asilimia themanini ya hao wanaoketi katika jengo hili usiku wa leo waliinua mikono yao kwa maombi. Inaonyesha, Bwana, ya kwamba hatuwezi tu kwenda bila Wewe. Hatuna budi kuwa Nawe, siku baada ya siku. Wewe ndiwe Uzima wetu, furaha yetu, afya yetu, nguvu zetu zinazotuhifadhi, tegemeo letu, kifungo chetu, ngao yetu kwa adui.

Nasi tusingaliweza kupiga vita hii ya maisha bila Wewe. Isingewezekana kabisa kwetu kufanya jambo hilo, nasi hatuna budi kukutegemea Wewe kabisa. Kwa kuwa, tunajua ya kwamba tunatembea katika nchi yenye huzuni na giza. Kila upande adui ametuvizia, kwa kuweka mitego na majaribu. Njia zetu, Bwana, zimejaa mitego ya adui, kutuhangaisha.

10 Na sasa sisi, pia, tunajua kwenye mwisho wa safari tuna lile bonde refu na lenye kivuli linaloitwa mauti tunalopaswa kupitia. Ee Bwana, ni nani angeishika mikono yetu wakati huo? Tunataka kukujua Wewe sasa Bwana. Tunataka kujua ya kwamba una mikono yetu nasi tuna mkono Wako, ya kwamba tunaweza kuwa na dhamana ile iliyotiwa nanga ili kwamba tutakapofikia wakati ule mkuu wa mwisho wa maisha yetu, unaoingia katika mlango ule unaoitwa mauti, ya kwamba tunaweza kusema pamoja na watakatifu wa kale, "Ninamjua Yeye katika nguvu za kufufuka Kwake, nami najua ya kwamba Yeye atakapoita, nitatoka katika wafu."

11 Sasa, Baba Mungu, tungeomba ya kwamba utazibariki haja zetu na kukutana kwetu. Bariki Maneno Yako; na kama nikisema lo lote ambalo lingekuwa kinyume na Neno Lako ama mapenzi Yako, Wewe ungali na nguvu za kufunga mdomo, kama Wewe ulivyofanya katika tundu la simba wakati Danieli alikuwemo. Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba ungefungua maskio na mioyo usiku huu, ya kwamba, na uumbe ndani yake njaa na kiu. Na waone kiu sana hata hawawezi kulala wala kupumzika mahali po pote hata yule Mfariji atakapokuja.

12 Tunaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho, katika vivuli vya Kuja Kwake. Na huko ndiko jumbe hizi zimeelekezwa, Bwana. Ni kusudi watu watahadhari, wapate onyo. Basi jalia, usiku huu, tuondoe tu lile ganda, sasa hivi, tuliweke kando ya benchi, tuseme, "Bwana Mungu, mimi ni chambo Chako. Jalia Roho Wako aumbike ndani yangu. Anifinyange na kunifanya kulingana na mapenzi Yako. Nitautoa moyo wangu, nguvu zangu, yangu yote kwa ajili ya kazi Yako."

13 Tusikie, Bwana. Sisi hatuko hapa tupate kuonekana, katika usiku huu wenye mvua. Hatuko hapa kwa kukosa tu mahali pengine pa kwenda. Tuko hapa kwa ajili ya kusudi moja lenye kicho, la wakfu na takatifu mioyoni mwetu, hiyo ni

kusema, kukukaribia Wewe, tukijua ya kwamba Wewe umeahidi kama tukikukaribia Wewe, Wewe ungetukaribia. Na hiyo ndiyo sababu tuko hapa. Yeye ajaye akiwa na njaa hatatoka akiwa na njaa. "Heri hao walio na njaa na kiu ya haki," kasema Yesu, "kwa kuwa watashibishwa." Na kama tukiomba mkate, hatutapokea jiwe. Tuna ahadi hiyo. Na kama tukiomba samaki, hatutapokea nyoka. Lakini, Mungu Baba yetu atatulisha kwa Mana ya Mbinguni, Neno Lake na Roho Wake ambaye anamshuhudia. Yajibu maombi yetu, Bwana, na haja zetu, tunapokungojea Wewe zaidi. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.

14 Sasa, ninyi ambao mnayaandika Maandiko haya, kama mngeweza kufungua pamoja nami Yohana Mtakatifu tena, sura ya 14, tunataka kuanza kwenye sura ya 14 ya Yohana Mtakatifu. Na hebu tuanze kwenye aya ya 14, Yohana Mtakatifu 14:14, na tusome tu sehemu ya Maandiko haya. Naam, katika haya mtapata fungu la maneno ninayotaka kuzungumza juu yake usiku huu.

15 Basi kumbukeni, ninyi ambao mna zile Biblia za herufi nyekundu, yako katika herufi nyekundu, haya ndivyo yalivyo. Ni Maneno ambayo Yesu Mwenyewe alinena, kwa hiyo basi tunaweza kuwa na uhakika ya kwamba itakuwa tu kama alivyosema Yeye. "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Lake halitashindwa kamwe."

Naam, tutasoma kutoka kwenye aya ya 14 ya sura ya 14.

*Mkiniomba Neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.*

Ni ahadi yenye baraka jinsi gani!

*Mkinipenda, mtazishika amri zangu.*

*Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;*

*Ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni . . .*

Naam, nyinyi ambao mngekuwa mnasoma kutoka kwenye Biblia ya Kiyunani, mngeliona jambo hili hapa, si . . . *Kuona* hapa linamaanisha "kufahamu." "Kwa kuwa ulimwengu haumfahamu." Hilo ni kweli kabisa. Hebu nilisome tena sasa.

*Ndiye Roho wa kweli; ambaye u- . . . kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua* (Nani? Mfariji), *maana anakaa kwenu,* sasa (wakati uliopo), *anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.*

Ni nini? Mfariji yule yule.

*Sitawaacha ninyi yatima; naja . . .*

Mtu ye yote anajua "naja" ni kijina cha nafsi.

*. . . naja kwenu.*

*Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena; bali* mta-. . .*bali ninyi mnaniona; na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.*

*Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu.*

Hapo ndipo patakuwa kiini cha wazo langu, bali tutasoma mbele kidogo. Hebu nisome hayo pia sasa, tena.

*Siku ile* (ile siku kuu, siku ya hukumu) *siku ile mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu.*

*Yeye aliye na amri* yangu, *na kuzishika, yeye ndiye anipendaye, naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.*

*Yuda (Siye Iskariote), akamwambia, Bwana, imekuwaje ya kwamba wataka kujidhihirisha kwetu, wala si kwa ulimwengu*?

Huo ni *kosmos*, "taratibu za ulimwengu." Kama una maandiko ya pambizoni pale, utaona. Yangu ni "g," na yanasema hapa, "*kosmos*, ama taratibu za ulimwengu." Hayo ni makanisa, na kadhalika, mnaona?

. . .*imekuwaje ya kwamba* utajidhihirisha *kwetu wala si* kwao? Unawezaje kufanya jambo hilo?

*Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu*; (amina!) *na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake.*

*Mtu asiyenipenda, yeye hayashiki maneno yangu*;. . .

Huenda wakayashika maneno ya kanisa; bali ni kuyashika maneno Yake, mnaona.

. . .*nalo* maneno *mnalosikia si langu, ila ni lake Baba aliyenipeleka.*

*Hayo ndiyo niliyowaambia wakati nilipokuwa nikikaa kwenu.*

*Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote* haya (hiyo ni kusema, Maneno Yake) *kuwakumbusha yote niliyowaambia.*

Mungu alimtuma Roho Mtakatifu kwa kusudi gani basi? Na aongeze baraka Zake kwa Neno Lake.

16 Yesu alisema, ya kwamba, "Siku ile mtatambua ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba Yangu, naye Baba ndani Yangu; nanyi mko. . .Mimi niko ndani yenu, nanyi ni ndani Yangu." Sasa, kama tutasema jambo hili . . .

17 Sasa, kumbukeni, hili litakuwa kwenye kanda.

Mfanyi biashara Mkristo, kutoka Louisville, alinipigia simu muda kidogo uliopita. Akasema, “Ni aibu, Billy, ya kwamba Jumbe hizi, kama ulivyosema usiku wa jana, haziwafikii watu elfu arobaini hapa badala ya mia moja na hamsini, ama mia mbili, watu mia tatu kwenye maskani yako madogo.”

18 Nikasema, “Bwana, katika miezi sita tangu sasa, kama Yesu akikawia, ulimwengu mzima utausikia huu.” Mnaona?

Hizo kanda zinaenda kila mahali ulimwenguni, mnaona, kila mahali. Kwa hiyo, basi, tunafundisha hapa kile tu tunachoamini kwamba ni Kweli, na kile tumekuta kwamba Mungu amethibitisha kwamba ni Kweli.

19 Sasa, kusudi, lilikuwa nini—kusudi la Mungu katika kumtuma Roho Mtakatifu lilikuwa nini? Sasa, ningeandika hilo, Yohana 14, kuanzia aya ya 14, na kusoma sura yote, kuweka msingi. Kusudi la Mungu, tunaona hapa, katika kumtuma Roho Mtakatifu, lilikuwa kusudi moja, ya kwamba Mungu Mwenyewe apate kuishi katika Kanisa Lake na kuendeleza mipango Yake kupitia kwa Kanisa. Kwamba, Mungu alikuwa katika Kristo, akiendeleza mipango Yake kupitia kwa Kristo; kutoka kwa Kristo, kuingia Kanisani, kuendeleza kazi Yake kupitia kwa Kanisa.

20 Sasa, tunajua Roho Mtakatifu ni nini. Tuliona, jana usiku, ya kwamba ni Mungu.

Sasa, tunapowazia juu ya Mungu, Baba, kama Yesu alivyonena hapa, Baba Yake; Mungu, Mwana, kama Yesu; Mungu, Roho Mtakatifu, kama tunavyomwita siku hizi. Naam, hiyo haina maana kwamba kuna miungu watatu mbalimbali. Ina maana kwamba kuna Mungu mmoja katika afisi tatu.

Hebu tulisema namna hii. Yote aliyokuwa Mungu, Yeye aliyamwaga katika Kristo, kwa maana Yeye alijitoa yote na kuyamwaga katika Kristo. “Naye Kristo alikuwa Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.” Yote aliyokuwa Yehova, Yeye aliyamwaga katika Kristo.

Nayo yote aliyokuwa Kristo, Yeye aliyamwaga katika Kanisa; si katika mtu mmoja, bali katika Mwili wote. Hapo, wakati tunapokutanika pamoja katika umoja, tuna Nguvu. Yote aliyokuwa Mungu, yalikuwa katika Kristo; na yote aliyokuwa Kristo, yako ndani yako.

“Kwa maana Mungu alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Timotheo wa Kwanza 3:16, kama mnayaandika. “Na bila shaka siri ya utauwa ni kuu: kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili, nasi tulimshika. Mungu, Yehova, aliyefanyika mwili, na kutembea duniani, nasi tulimwona kwa macho yetu.”

21 Mwajua, katika sura ile ile, ya Yohana 14, Filipo alisema, “Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha.”

22 Yesu akasema, “Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, Filipo, msinijue? Mkishaniona Mimi, mmemwona Baba Yangu. Basi wewe waniambiaje, ‘Utuonyeshe Baba.’?” Mungu alifanyika mwili.

23 Basi hili hapa. Baba alikuwa Mungu juu yenu, tunasema. Tumekuwa tangu Adamu. Mungu, Baba, alikuwa juu ya Musa na wana wa Israeli, katika Nguzo ya Moto. Halafu, Mungu pamoja nasi, katika Kristo; akatembea pamoja nasi, akanena pamoja nasi, akala pamoja nasi, akalala pamoja nasi. Mungu juu yetu; Mungu pamoja nasi; na sasa Mungu ndani yetu. Yote aliyokuwa Mungu, yaliingizwa katika Kristo; yote aliyokuwa Kristo, yaliingizwa katika Kanisa.

Ni nini? Mungu akitenda kazi ndani yako. Po pote ulimwenguni ambapo angetaka kukuita, uko papo hapo, akifanya kazi pamoja nawe kutekeleza mapenzi Yake mema. Jinsi tunavyopaswa kumshukuru Mungu kwa sababu hiyo! Mungu, Roho Mtakatifu, anatumwa kwa kusudi la Mungu kuishi katika Kanisa Lake, akitenda kazi katika kila wakati, akitekeleza mapenzi Yake ya Kiungu.

24 Watu wanapokufanyia mzaha, hawakufanyii mzaha, wao wanamfanyia mzaha Yeye aliyekupeleka. Kwa hiyo Yesu alisema, “Heri nyinyi watakapowanenea kila neno baya, kwa uongo, kwa ajili ya Jina Langu. Heri ninyi.” Halafu, tena, “Wote wanaoishi maisha ya kitauwa katika Kriato Yesu wataudhiwa.”

Kwa maana, wakati Mungu alipojitambulisha katika Kristo, wao walimchukia. Ni nani waliomchukia Yeye, zaidi? Kanisa. Kanisa lilimchukia, zaidi. Walimchukia kuliko m—mlevi. Walimchukia kuliko watu wengine wote. Kanisa ndilo lililomchukia Yeye. Kwa hiyo, basi, unapoona *kosmos*, “Taratibu za ulimwengu, ulimwengu haukumjua Yeye,” maana yake ni, “kanisa,” kama linavyojiita, “halikumjua. Alikuja Kwake, wala walio Wake hawakumpokea.”

“Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina Lake.” Loo, jinsi tunavyopaswa kumpenda na kumwabudu Yeye! Kusudi la Mungu, akitaka kuwa na ushirika!

25 Kama vile, kabla hatujaliacha somo hilo, hebu tulitumie hili; katika siku za Ruthu, katika sheria ya ukombozi, baada ya Naomi kuondoka nchini, kwa sababu ya majaribu, nyakati za shida. Yeye alienda katika nchi ya Wamoabi, ambao walikuwa tu Wakristo wenye uvuguvugu na wa kawaida. Kwa maana, Wamoabi walitoka kwa binti wa Lutu, nao walijiita waamini, na walikuwa wamechanganyikiwa. Ndipo basi mumewe akafa, na wanawe wawili wakafa. Nao walipokuwa wakienda zao nyumbani, Naomi . . . Ruthu na Naomi, wakienda zao nyumbani, ninino yake . . . Mmoja wa wakwe zake, Orpa, yeye alisema angerudi nchini mwake, kwa miungu wake, na kanisa lake, na

kwa watu wake. Ndipo Naomi akajaribu kumfanya Ruthu arudi, lakini akasema, "Watu wako ni watu wangu. Mungu wako ni Mungu wangu. Utakapokufia, nitakufia huko. Utakapozikwa, nitazikwa huko. Nami sitarudi."

26 Hapo ni wakati mtu anapopata ono. Haileti tofauti yo yote watu wake walivyosema. "Utaenda kule uwe mtakatifu anayejifingirisha ama cho chote kile." Hilo halikuleta tofauti yo yote kwa Ruthu. Kulikuweko na kusudi la Mungu kutimizwa.

27 Na kadiri unavyoona njaa ya Roho Mtakatifu usiku huu, ni kitu fulani ndani yako, kinachovuta, ya kwamba kusudi fulani la Mungu katika maisha yako halina budi kutimizwa, kama tu lilivyotimizwa kwa Ruthu.

28 Hadithi hiyo ni nzuri sana! Siwezi tu kuiacha, kwa muda kidogo. Mnajua sheria ya ukombozi, ya kwamba wakati Boazi . . . Mnajua hadithi ya jinsi Ruthu alivyookota masazo ya masuke kondeni kisha akapata kibali kwa Boazi. Na kabla hajaweza kumwoa, ilimbidi kukomboa yote ambayo Naomi alikuwa amepoteza. Na mtu pekee ambaye angeweza kukomboa mali ya Naomi yaliyopotea, katika sheria ya ukombozi, alikuwa ni jamaa wa karibu; ilimbidi awe jamaa kabla hajaweza kukomboa. Na huyo alikuwa jamaa wake aliye karibu sana. Naye ilimbidi kutoa ishara hadharani, nje ya lango, ama kukiri hadharani ya kwamba alikuwa amekomboa yote Naomi alikuwa amepoteza. Basi Boazi alifanya jambo hilo kwa kuvua kiatu chake mbele ya wazee, na kusema, "Kama kuna mtu hapa aliye na cho chote ambacho ni mali ya Naomi, leo hii nimekikomboa!"

29 Na hivyo ndivyo alivyofanya Mungu, alifuata sheria Zake Mwenyewe. Mungu hawezi kufuata, kuwapa sheria moja mkaifuate kisha Yeye afuate nyingine. Yeye hufuata sheria Zake Mwenyewe. Ndipo, Mungu, kusudi alikomboe kanisa lililopotea, ulimwengu uliopotea, viumbe vyote vilivyopotea; Mungu, ambaye hana kikomo katika Roho, kuikomboa jamii iliyopotea ya binadamu, Mungu Mwenyewe alifanyika jamaa aliye karibu, Mtu, Mwana aliyemuumba katika tumbo la uzazi la Mariamu. Halafu Yeye akafanya ishara, ama ushuhuda; nje ya milango ya Yerusalemu. Yeye aliinuliwa kati ya mbingu na nchi, kisha akafa, na kukomboa kila kitu. Na katika kutokwa na damu, Yeye alilitakasa Kanisa ili kwamba Yeye Mwenyewe apate kuishi mle ndani, na kufanya ushirika na kushiriki nalo, ile sehemu iliyopotea ya ushirika tangu bustani ya Edeni ambamo Mungu alishuka kila jioni, wakati wa kanisa.

Uliona, Mungu alishuka akaja wakati wa jua kupunga, machweo ya jua. Kuna kitu fulani kuhusu wakati inapoanza kuwa giza, watu wanafikiri juu ya kanisa pamoja na Mungu; Wakristo. Unaona jua likitua, unatambua ya kwamba jua lako linatua.

30 Basi katika wakati wa jua kupunga Yeye angeshuka na kushiriki pamoja nao. Ndipo hapo akapoteza ule ushirika, kwa maana dhambi isingemruhusu kufanya jambo hilo.

Halafu basi alifanyika mwili akakaa kwetu, kusudi apate kurudi tena kwa mwanadamu, na kuishi katika mwanadamu, na kumrudisha mwanadamu katika hali ya ushirika pamoja Naye tena, na kumrudishia haki zake alizopewa na Mungu. Hivyo ndivyo alivyofanya.

31 Hilo ndilo kusudi la Roho Mtakatifu. Ni Baba, tena, Mungu Baba akiishi ndani yako, akitekeleza mipango Yake, kumaliza mpango Wake wa ukombozi; akifanya kazi kupitia kwako, akikufanya mfanya kazi pamoja Naye; akikupa mahali fulani, akikupa sehemu fulani kwa ajili ya ndugu na dada yako walioanguka; akikupa wewe Roho Wake na upendo Wake, wa kwenda kuwatafuta waliopotea, kama alivyofanya katika bustani ya Edeni. "Adamu, Adamu, uko wapi?" Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu anavyomfanyia mwanamume ama mwanamke. Hapo Yeye anapougusa moyo wao na kupata kikao Chake, kuna kiu na kuona njaa kwa ajili ya watu waliopotea.

Hiyo ndiyo shida ya mikutano siku hizi. Hamna mguso wa kutosha wa Roho mle, kuenda kawatafuta waliopotea na wanaokufa. Zaidi sana ni kwa ajili ya kujifanyia jina, ama kanisa, ama jengo, ama madhehebu, badala ya mpango wa kuwavuta watu. Ni jambo la kusikitisha jinsi gani! Tungeweza kukaa juu ya jambo hilo sana.

Mungu alijimwaga Mwenyewe katika Kristo. Kweli.

32 Kristo alijimwaga katika Kanisa. Kwa hiyo, sasa angalia, "Siku ile mtatambua ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba Yangu, nanyi mko ndani Yangu, Nami niko ndani yenu. Siku ile mtajua jambo hilo." Kwa kuwa, jambo lote ni mpango mmoja wa ukombozi ukishuka, kwamba Mungu anarudi kuishi ndani, na kuishi pamoja, na kushiriki pamoja na watu Wake, kama alivyofanya hapo mwanzo.

Naam, basi, mara anapolifanya Kanisa Lake kuwa katika hali ya kuzungumza, anapoliweka Kanisa Lake mahali ambapo anaweza kujiingiza ndani, na kupenda, na kushawishi, na kushiriki, basi Edeni itatokea. Atalirudisha Kanisa Lake mahali ambapo li—lilipomwacha Yeye, kurudi kwenye Edeni tena, mahali pale lilipoangukia. Hilo, sasa... Hapo ndipo lilipoanza mara ya kwanza, ama lilipoangukia. Hapo ndipo litakaporudishwa moja kwa moja, pamoja na kila kibao safi cha ukombozi, kuwarudisha moja kwa moja mahali hapo tena.

33 Kanisa limekuwa ulimwenguni kwa muda fulani. Nalo Kanisa, kweli, baada ya yale matengenezo, ya miaka elfu moja mia tano ya nyakati za giza... Luther alikuwa mtengenezaji wa kwanza kutokea baada ya kile kipindi cha mitume. Halafu Luther alipojitokeza, Mungu alimwaga Roho kidogo na

kuimwaga juu ya Kanisa, katika kuhesabiwa haki. Halafu basi katika siku za Wesley, Yeye aliimwaga sehemu Yake ndogo zaidi, katika utakaso. Na kadiri wakati umeendelea mbele, hata kwenye wakati wa mwisho, Mungu amekuwa akilijaza Kanisa Lake. Tazama tu kila mahali uone kama hiyo ni Kweli, ama si kweli.

34 Angalia wakati wa Kiluteri, ninyi ambao husoma historia, angalia ufufuo wao na yale waliyofanya. Angalia jinsi ufufuo wa Wesley ulivyokuwa mkuu zaidi, jinsi walivyokuwa na nguvu nyingi zaidi, bali katika uchache. Angalia katika siku za Kipentekoste, ufufuo waliokuwa nao wakati huo, jinsi ulivyokuwa mkuu, ukasambaa kote.

35 Pia, *Mgeni Wetu Wa Jumapili*, lile gazeti la Kikatoliki, lilikiri ya kwamba Wapentekoste walipata waongovu milioni moja na mia tano elfu katika mwaka mmoja, wakayashinda makanisa mengine yote pamoja. Katoliki iliongezeka tu, walidai, milioni moja. Katika gazeti lao la *Mgeni Wa Jumapili*, gazeti linaloitwa *Mgeni Wa Jumapili*, lilitoa tamshi kwamba Wapentekoste waliwashinda.

Basi, kumbukeni, kuongoka kwa Kipentekoste ni kuongoka kwa kujazwa na Roho Mtakatifu. Katika uchache, kwanza, huko vichochoroni huko nje, wakiwa na—na gita ya kale. Na hao wanawake hata hawangaliweza kununua jozi ya soksi ndefu. Wakilala kwenye njia za reli, huku wakiokota mahindi na kuyasaga, na kuwaokea watoto wao mikate. Lakini matokeo yake ni nini? Kanisa lenye nguvu sana lililoko ulimwenguni leo, si katika macho ya ulimwengu, bali katika macho ya Mungu, kwa sababu yeye analithibitisha kwa yale anayowafanyia. Yeye anajimwaga ndani yao, akimmwaga Huyo.

36 Angalia sasa kile kilichotokea, Mungu akijimwaga ndani yao. Sasa Kanisa limefikia mahali, kutoka kwa Luther, Wesley, na ufufuo umewaka moto kwa Wapentekoste; na sasa umeingia katika wakati huu tunaoishi sasa, kwa Roho Mtakatifu yule yule, kwa wingi zaidi. Naam, wakati Waluteri kule nyuma waliokolewa, walipokea sehemu ya Roho Mtakatifu. Wakati Wamethodisti walitakaswa, hiyo ilikuwa ni kazi ya Roho Mtakatifu. Mnaona, ilikuwa ni sehemu ya Roho Mtakatifu. "Wao pasipo sisi hawakamilishwi," yasema Maandiko. Mnaona?

37 Naam Mungu, kwa kuwa Nuru imeanza kung'aa katika siku za mwisho, Yeye anatutarajia, jambo kubwa kutoka kwetu sisi. Kwa kuwa, "Palipotolewa mengi, mengi hutakiwa." Kwa hiyo atatudai mengi zaidi kuliko alivyofanya kwa Waluteri ama Wamethodisti, kwa maana tunatembea katika Nuru kuu zaidi, kwa Nguvu kuu zaidi, pamoja na—na ushuhuda mkuu kuliko waliokuwa nao. Naam, tuna ushahidi mkuu zaidi wa ufufuo. Tuna mambo yaliyo thabiti zaidi, yenye uhakika kuliko waliyokuwa nayo.

38 Lakini ni kama tu nilivyosema kwenye chuo cha Kiluteri, si muda mrefu uliopita.

Wao walisema, “Tuna nini sisi?”

Nikasema, “Mtu fulani alipanda shamba la mahindi. Majani ya kwanza yakachipuka, ndipo akasema, ‘Bwana ashukuriwe kwa ajili ya ma—mazao ya mahindi!’ Kwa uwezekano, alikuwa nao, bali alikuwa nao tu katika hali ya mwanzoni. Bali muda si muda likawa ubua.”

Kisha kishada kikatokea, ambacho kilikuwa Wamethodisti.

39 Kama utaangalia maumbile, utamwona Mungu akitenda kazi. Kuna siri iliyo mle ambayo hata inaambatana na huduma yangu. Mnaona? Huko, kuangalia maumbile, kuona jinsi yanavyofanya, ni wakati gani ni saa ipi, unaweza kuona unakoishi. Angalia huo wakati.

40 Naam, halafu, Wamethodisti, wao walikuwa ni vishada. Waliangalia huko nyuma kwa Waluteri, kasema, “Tuna kutakaswa; hamna kitu ndani Yake.”

Muda si muda, kutoka kwenye mbelewele hiyo, kutoka kwenye Wamethodisti, kukaja chembe ya . . . suke la mhindi. Hiyo ilikuwa Pentekoste.

Haya basi, kuhesabiwa haki, hatua moja Yake. Kutakaswa, hatua nyingine Yake. Roho Mtakatifu, hatua nyingine Yake; Pentekoste. Luther, Wesley, Pentekoste.

41 Sasa Pentekoste inafanya nini? Ninailinganisha, kwa sababu, katika Pentekoste, ilirudisha, si kijani kibichi, si kishada, bali . . .

Ile chembe haiwezi kukiambia kishada, “Sina haja nawe.” Wala, kishada hakiwezi kuliambia ja—jani, “Sina haja nawe,” kwa maana uhai ule ule uliokuwa katika jani ulikifanya kile kishanda. Uhai ule ule uliokuwemo katika kishanda ulilifanya lile suke.

Na kanisa la Kiluteri ndilo lililolifanya kanisa la Kiwesley. Kanisa la Kiwesley ndilo lililolifanya la Kipentekoste.

Lakini, Pentekoste, ni nini? Ni kurudishwa kwa chembe ile ile iliyoingia ardhini hapo mwanzo, ikileta utimilifu wote wa Nguvu za Kipentekoste, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, mnaona, katika siku za mwisho. Loo, ni jambo kubwa sana, la kuangalia, kuamini na kuangalia.

42 Naam, katika wakati huu tunaoishi, wakati huu, umepita wa Pentekoste.

Pentekoste imejiandaa kama madhehebu, na kuanza kuiga sana juu ya madhehebu, “Sisi ni *hiki*, nasi ni *kile*.” Hiyo ni maumbile tu. Huwezi kuizuia kamwe. Ni maumbile. Wao watafanya jambo hilo. Imekusudiwa, kwamba watafanya hivyo.

Bali kanisa limesonga mbele. Limeingia katika jambo kuu zaidi, lenye nguvu zaidi. Ni kule kurudishwa kwa vipawa.

Na Wapentekoste wengi hawaamini katika kuponya Kiungu, huduma ya Malaika, na nguvu za Mungu. Wapentekoste wengi huita maono haya ninayoona, "ibilisi." Madhehebu mengi hata hawatajihusisha Naye kamwe, katika Pentekoste. Mnaona, tumesonga mbele ya hapo. Kama tu vile Wamethodisti walivyowaita Wapentekoste, "wenye kichaa," kwa ajili ya kunena kwa lugha. Kama tu vile Waluteri walivyowaita Wamethodisti, "wenye kichaa," kwa kupiga makelele. Mnaona?

Lakini yote ni kutokea kwa Roho Mtakatifu, hata Kanisa lote lililo kuu linajazwa kabisa, na kushindiliwa kabisa, haleluya, [Ndugu Branham anapiga-piga mimbara mara mbili—Mh.] kwa nguvu kuu za Mwenyezi Mungu. Hata, imefikia wakati ambapo kazi zile alizofanya Yesu zinajidhihirisha zenyewe moja kwa moja Kanisani sasa. Tuko karibu, enyi marafiki.

43 Hebu nisimame hapa, kwa muda kidogo tu, kupata kusudi la Mungu kumweka Roho Mtakatifu Kanisani, niwape mfano mwingine ili kwamba mpate kujua. Huko nyuma katika Agano la Kale, wakati m—mtoto . . .

Mtu alipojitengenezea nyumba. Alimchukua bibi-arusi wake, hilo ndilo jambo la kwanza.

Ndipo akawa mtu mashuhuri, kama madhehebu. Hilo lilikuwa jambo zuri.

Jambo la pili lililotokea, mtoto akazaliwa katika nyumba hiyo. Huo ndio wakati Roho Mtakatifu, mnaona, roho mwingine akaingia, ambaye alikuwa mwana. Mwana huyo, hakuwa na mamlaka yote, wala hakuwa mrithi hata alipofikia kwenye umri fulani. Naye ilimbidi ajaribiwe, kwanza. Naam.

Halafu basi wao walikuwa na sheria ya kufanywa mwana mwenye mamlaka. Kwenu wahudumu, "kufanywa wana mwenye mamlaka," ndiko ninakozungumzia sasa, mnaona, ndipo alipofikia mahali ambapo alifanywa mwana mwenye mamlaka. Yesu alitoa mfano mzuri wa jambo hilo, kwenye Mlima wa Kugeuzwa.

44 Kama nilivyosema, Mungu kamwe hatatoka nje ya sheria Zake kufanya jambo lo lote.

Kama una kisima kinachobubujika maji kwenye kilima *hiki*, kikiyarusha maji kila mahali hewani. Na kwenye kilima hiki kingine *hapa*, una mimea inayoungua. Unaweza kusimama kwenye kilima hiki na kupiga makelele, "Jamani, maji, kimbia hapa ukainyunyizie mimea yangu! Jamani, maji, nenda kwenye mimea yangu!" Hayatafanya hivyo kamwe. Bali kama ukifanya kazi kulingana na kanuni za uvutano, unaweza kuinyunyizia mimea hiyo.

45 Kama una mgonjwa aliye hapa, ama mwenye dhambi aliye hapa, ama mtu anayetaka kuwa sawa, hawezi kuacha kunywa pombe, hawezi kuacha kuvuta sigara, hawezi kuacha kutamani kimwili na kadhalika. Kama utafanya kazi tu kulingana na sheria za Mungu, umruhusu Roho Mtakatifu aingie mle ndani, basi yeye si wa nafsi yake mwenyewe. Yeye, yeye ataacha kitu hicho, kwa maana Roho Mtakatifu anamtawala. Bali huna budi kufanya kazi kulingana na sheria za Mungu, taratibu za Mungu.

46 Basi, katika Agano la Kale wakati mtoto huyu alipozaliwa, walichunguza, waone jinsi alivyoenenda, mwenendo.

Ndipo babaye, akiwa mfanyi biashara mashuhuri kwa wakati huu, labda akiwa kwenye umri wa miaka arobaini ama hamsini, yeye, mwenyewe, hakuwa na wakati wa kumfundisha mtoto huyu mchanga, kwa hiyo akamchukua... Katika siku hizo wao hawakuwa na shule za umma kama walivyo nazo sasa, kwa hiyo wakamchukua waliyemwita "mwalimu" ama "mlenzi," mwalimu wa shule. Naye mwalimu huyu wa shule alikuwa ndiye bora sana ambaye angeweza kumpata, ili kwamba aweze kuwa mwaminifu na kumwambia babaye ukweli wa mambo.

47 Halafu mvulana huyu alipofikia umri fulani, tuseme, alikuwa amekomaa. Kama mtoto huyo alikuwa tu muhuni, hafai, hakujali biashara za babaye; yote aliyofikiria yalikuwa ni kumbembana na kuzurura na wanawake, ama—ama kunywa pombe, ama kucheza karata, ama mbio za farasi; mvulana huyo daima angekuwa ni mwana, bali hakuwekwa kamwe katika mahali ambapo angekuwa mrithi wa yote aliyokuwa nayo babaye.

Bali kama alikuwa mvulana mzuri, na alikuwa akifanya shughuli za babaye, kisha akathibitishwa kwamba ni mvulana anayestahili, basi walifanya sherehe. Walimchukua mvulana huyo wakampeleka huko nje mitaani wakamvalisha vasi jeupe, kisha wakamweka kwenye jukwaa ili kwamba jiji nzima liweze kumwona. Wakafanya karamu na sikukuu, ndipo babaye akafanya sherehe ya kufanywa mwana mwenye mamlaka. Akamwadhimisha mwanawe katika biashara yake, ndipo huyo mwana alikuwa sawa na baba yake. Kwa maneno mengine, kama ingalikuwa ni siku hizi, jina la huyo mwana kwenye hundi lilikuwa sawa na la babaye.

48 Sasa angalia alilofanya Mungu. Wakati Mwanawe alipozaliwa, Yeye alimwacha aende kwa muda wa miaka thelathini, akimjaribu, akimchunguza. Kisha akampa miaka mitatu ya majaribu magumu. Ndipo mwishoni mwa yale majaribu magumu, wakati alipoona ya kwamba Mwanawe alikuwa anafanya kazi ya Babaye; Mlima wa Kugeuzwa, Kitabu cha Luka; Yeye alikamchukua Petro, Yakobo, na Yohana, mashahidi watatu, akaenda juu ya mlima, ndipo hapo Mungu

akatekeleza sheria ya kufanywa mwana mwenye mamlaka. Yeye. . . Wao waliangalia juu wakamwona Yesu, nazo nguo Zake ziling'aa zikawa nyeupe kama umeme. Kisha Wingu likamfunika, na Sauti ikatoka katika lile Wingu, ikasema, "Huyu mi Mwanangu nimpendaye; msikieni Yeye. Nitaketi chini sasa, nisiwe na lingine la kusema. Asemayo ni sheria na ni Kweli."

49 Sasa kanisa limepitia kwenye itikadi hizo. Limeoalewa kule nyuma, muda mrefu uliopita, na kufanyika madhehebu, shirika. Lakini, mnaona, kule Kuzaliwa kulitoa kitu kingine. Na sasa limefikia mahali ambapo kanisa la Kipentekoste, likiwa na kule Kuzaliwa upya, limechunguzwa na kujaribiwa, na sasa linafikia mahali . . . Mungu hashughuliki na Kanisa kama tu madhehebu. Yeye hashughuliki na Kanisa kama ku—kundi la watu.

Yeye hushughulikia kanisa kama mtu binafsi, kila mtu mmoja mmoja Kanisani. Na sasa imefikia wakati. . . Na si siri; sisi sote tunaona jambo hilo. Mtu anapothibitisha, naye Mungu anampenda, Yeye anamchukua anampeleka mahali fulani peke yake. Hapo mbele ya Malaika anamfanyia jambo fulani! Yeye anamwinua pale Mbele za Mungu, na kumpa vipawa, na kumjaza, na kumweka huko nje. Huo ndio wakati tunaoishi.

50 Roho Mtakatifu yule yule aliyewaokoa Waluteri; aliyewatakasa Wamethodisti; aliyewabatiza Wapentekoste; sasa anatayarisha kule Kuja kwa Bwana Yesu. Wakati, utakapokuwa na nguvu sana, Mwili huo, utaingia katika Kundi hili, Kanisa, hata litawavuta hao wengine kutoka kaburini. Kutakuwako na ufufuo. Hilo ndilo kusudi la Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni nini? "Pasipo sisi wao hawawezi kukamilishwa." Wao waliishi katika siku moja, chini ya jambo hilo. Sisi tunaishi katika siku nyingine.

"Adui anapokuja kama mafuriko, mimi nita-. . . Roho wa Mungu atainua beramu dhidi yake." Mnaona? Tuko katika siku fulani sasa . . .

51 Kule nyuma, wao hawakuwa werevu nusu ya walivyo siku hizi. Wao wasingeweza kuunda bomu la atomiki wala motokaa. Wao hawakuwa na sanyansi na mambo tuliyo nayo leo, lakini, na mambo ya vitu vya kisiri; kujaribu kusema mwanadamu alipulizwa pamoja, kwa baadhi ya mavumbi na kadhalika, na kufanya utafiti na kujaribu kuthibitisha jambo hilo, kuwafanya watu makafiri.

Lakini sasa, wakati tunapomhitaji, Roho Mtakatifu anainua beramu. Ni kitu gani? Yeye anamwaga Roho Yake. Ndipo, wale wanaopumzika kule ng'ambo kaburini, ama chini ya madhabahu ya Mungu, kama yanavyosema Maandiko, wakilia, "Hata lini, Bwana? Hata lini? Ni muda gani zaidi?" Mungu anatungojea mimi na wewe. Kanisa linatungojea mimi na wewe. Wakati wa kufanywa wana wenye mamlaka, wakati

Mungu anapoweza kumwaga ndani yetu utimilifu Wake, Nguvu Zake, ufufuo Wake, wakati Kanisa na Kristo wanafanana sana hata Kristo anaonekana mbele yetu, na kuwafufua wafu, nasi tunanyakuliwa.

52 Sasa tutasema, tutawaonyesha baada ya kitambo kidogo, ya kwamba ni wale tu waliojazwa na Roho Mtakatifu watakaonyakuliwa. "Kwa kuwa hao wafu wengine hawakuwa hai kwa muda wa miaka elfu moja." Hiyo ni kweli. Ni wale watu tu waliojazwa na Roho Mtakatifu walionyakuliwa. Naam, Mungu alitoa Roho Wake Mtakatifu . . .

53 Nina Andiko lingine hapa, katika Yohana 14:12. Hilo ni Andiko linalojulikana sana na watu wote hapa maskanini.

> "*Amin, amin, nawaambieni, yeye aniaminiye mimi . . .*"

Naam, msiache neno hilo "aniaminiye" kwa namna fulani liwarudishe nyuma. Katika kanisa la kawaida, kasema, "Naam, ninaamini. Hakika, ninaamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu." Ibilisi anaamini jambo lilo hilo. Hiyo ni kweli kabisa. Biblia ilisema yeye anaamini.

Lakini Maandiko yanasema, katika Yohana, ya kwamba, "Hapana mtu anayeweza kumwita Yesu Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu." Wewe, kweli, kwa Maandiko . . . Hebu nisimame hapa kwa muda kidogo tu, kabla sijamaliza kusoma. Hujaongoka bado mpaka umempokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli.

54 Wewe unaamini "hata." Roho Mtakatifu amenena nawe, nawe umemkiri Yeye hadharani. Ibilisi ana jambo lile lile. "Ninamwamini Yeye kuwa ni Mwana wa Mungu." Vivyo hivyo ibilisi naye. Bali unatembea kuelekea Kwake.

Wakati, Petro alikwisha kuitwa na kuhesabiwa haki, kwa kumwamini Bwana Yesu Kristo; na katika Yohana 17:17, Yesu aliwatakasa kwa Neno, kwa maana Neno lilikuwa ni Kweli. Naye alikuwa Neno. Yohana 1, inasema, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili, akakaa kwetu." Yeye alikuwa Neno, kwa hiyo Yeye akawatakasa. Akasema, "Baba," akinena kwa Roho aliyekuwa ndani Yake, "Ninawatakasa kwa Neno," Yeye Mwenyewe, kwa kuweka mikono Yake juu yao. "Neno Lako ni Kweli." Yeye kwa urahisi alimnena akawa, katika tumbo la uzazi la mwanamke; loo, haiwezekani kabisa kwa Yeye kuwa namna nyingine yo yote ila Neno hili la Mungu kumfanya Yeye adhihirike. "Mimi ninakwatakasa."

55 Yeye aliwapa nguvu juu ya pepo wachafu. Wakatoka wakaenda. Aliweka majina yao katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Kisha akawatuma nje, Yohana . . . Mathayo 10, na kuwapa nguvu juu ya pepo wachafu; kuwatoa pepo wachafu,

na kufanya kazi, na kadhalika. Nao wakarudi, wakifurahi, kasema, “Hata pepo wachafu wanatutii.”

Akasema, “Msifurahi kwa kuwa pepo wanawatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa katika Kitabu.” Naye Yuda alikuwa pamoja nao. Mnaona jinsi anavyoweza kusogea karibu; moja kwa moja kupitia kuhesabiwa haki, aingine moja kwa moja katika utakaso. Bali alionyesha nuru yake wapi? Alijidhihirisha wapi? Kabla ya Pentekoste, alionyesha rangi zake.

56 Angalia, roho huyo atakuwa wa kidini tu na mtawa na mtakatifu awezavyo kuwa, hata inapofikia kwa Roho Mtakatifu, nao watakatiza papo hapo. Huyo ni roho huyo (hivi hamwezi kumwona akiinuka?) akisogea, yule mpinga Kristo. Naye Yesu alisema, wangefanana sana, katika siku za mwisho, ingewapoteza walio Wateule kama yamkini.” Lakini, kumbukeni, walio Wateule ndio tu watakaoliona jambo hilo.

Mungu huita kwa uteuzi. Ninyi, hivi hamna furaha kwamba ninyi ni mmoja wao? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hivi ninyi, watu hapa usiku wa leo, mkijua ya kwamba kitu fulani moyoni mwenu kinavuta, “Ninamtaka Roho Mtakatifu huyo. Ninakutaka, Bwana, moyoni mwangu”? Hiyo ni kwa sababu Mungu aliweka jina lako katika Kita cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alisema jambo hilo.

“Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu,” Yesu alisema, “asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote wanijiao Mimi, nitawapa Uzima wa Milele.” Uzima wa Milele ni nini? Roho Mtakatifu. “Uzima wa Milele,” chukua neno hilo uliangalie katika ya Kiyunani, nayo ilisema, *Zoe*. Zoe ni Roho Mtakatifu. “Wote alionipa Baba Yangu watakuja Kwangu. Na wote wanijiao Mimi, nitampa Roho Mtakatifu, Nami nitamfufua katika siku ya mwisho. Nitafanya hivyo,” yeye alisema. Hakuna cha kama wala na juu yake. “Nitawapa. Wote wajao; nami nitawapa Uzima wa Milele.” Hana budi kufufuka, kwa kuwa ana Uzima wa Milele. Hana budi kuja. Hawezi kufa kama vile Mungu asivyoweza kufa.

57 Loo, marafiki wangu wapendwa kutoka kila mahali humu nchini na katika jiji hili dogo, laiti ninagliweza, kwa sauti yangu ya kibinadamu, kuweka ndani ya moyo wenu umuhimu wa kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, ungekuwa ufunuo wa ajabu sana uliowahi kuwa nao maishani mwako. Kuona vile . . . Huna budi kufanya jambo hilo.

Hebu niweke hilo wazi, kuhusu, “Hujaongoka.”

58 Petro alikuwa ameokoka. Alimwamini Bwana, akamfuata. Yesu alimwambia yeye alikuwa nani, akamfanya amfuate Yeye. Akampa nguvu juu ya pepo wachafu na kumtakasa. Bali baada ya hayo yote, kisha akawa mnenenaji mkuu wa hilo kundi;

kama vile Wakatoliki wangetaka kuita jambo hilo, “askofu wa kanisa, ama papa,” ama cho chote kile, kiongozi wa kanisa; hata hivyo Yesu alisema, kwenye ule usiku wa kusalitiwa Kwake, “Unanipenda Mimi, Petro?”

Naye akasema, “Bwana, unajua nakupenda.”

Akasema, “Lisha kondoo Wangu.” Alisema jambo hilo mara tatu.

Kisha Petro akasema, “Unajua nakupenda, hata nitaambatana Nawe hata mwi—mwisho, nami nitaambatana Nawe hata mautini,” na kadhalika.

59 Akasema, “Kabla jimbi hajawika mara tatu, uta-. . . kabla jimbi hajawika, utakuwa umenikana Mimi mara tatu.” Akasema, “Lakini, Petro, nimekuombea.” Sikilizeni. Hayo hayatoshi. “Nimekuombea. Na baada ya kuongoka, basi waimarishe ndugu zako.”

“Baada ya kuongoka.” Yeye alikuwa amepiga makelele. Alikuwa labda amecheza katika Roho. Yeye, alikuwa amefanya kila namna ya mambo, bali hakuwa amempokea Roho Mtakatifu bado. “Baada ya kuongoka, basi waimarishe ndugu zako,” hilo ni kweli, “kutekeleza mpango Wake.”

60 Basi hebu nimalize kusoma Yohana 14:12. Sasa, katika sura ya 14 na aya ya 12, Yesu alisema, “Amini, amin, nawaambia, yeye aniaminiye. . . ” Nawe huwezi kuamini. . . “Aniaminiye Mimi.” Unaweza kuamini *katika* Yeye. Ni wangapi wanafahahamu jambo hilo, semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.]

61 Mnakumbuka, katika Matendo 19. Nachukia kuachia jambo hili hapa, bali sina budi kulisema linavyonijia mimi. Katika Matendo sura ya 19, wakati mhubiri huyu wa Kibatisti, ambaye alikuwa mwa—mwanasheria na ameongoka, naye alikuwa akihubiri na kuwafanya watu waokoke. Nao walikuwa na furaha kuu, wakifurahi tu na kufanya shangwe, wakiwa na mkutano. Matendo 18, Akuila na Prisila, tulirejea kwa jambo hilo jana jioni, nao walikuwa wamekwenda kumwona. Na yote waliyojua alikuwa mtu mashuhuri, tena alikuwa mwanafunzi. Naye alikuwa akithibitisha kwa Biblia ya kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, akijua tu ubatizo wa Yohana. Hakujua ubatizo wa Roho Mtakatifu bado. Kwa hiyo akasema . . .

Akuila na Prisila, mwanamume yule pamoja na mkewe, maskini watengenezaji wa hema; ambapo, Paulo alikuwa mtengenezaji wa hema, pia. Nao wakampokea Roho Mtakatifu chini ya mafundisho ya Paulo. Wakasema, “Tuna maskini ndugu fulani anayekuja hapa. Hebu azungumze nasi kidogo juu ya jambo hilo.”

Basi Paulo alipokuja na kumsikia akihubiri, alijua alikuwa mtu mashuhuri, alisema, "Je! mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

Wao wakasema, "Hatujui kuna . . . kama kuna Roho Mtakatifu ye yote."

Akasema, "Basi mlibatizwaje," ama neno halisi la Kiyunani hapo ni, "mlibatizwa namna gani?"

Wao wakasema, "Tayari tumebatizwa na Yohana Mbatizaji."

62 Sasa angalia alivyosema Paulo. Paulo alisema, ya kwamba, "Yohana kweli alibatiza kwa ajili ya toba; si kwa ondoleo la dhambi, bali kwa toba, akisema, hivyo ndivyo mlivyoamini."

Unapomkubali Kristo kama Mwokozi wako binafsi, unaamini *ukielekea* kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu. Huo si ubatizo wa Roho Mtakatifu, ndugu zangu Wabatisti wapendwa. Ni kosa.

Ndugu fulani aliniambia juzijuzi, kasema, "Ndugu Branham," ama hivi majuzi, miezi kadha iliyopita, akasema, "Ndugu Branham, Ibrahimu alimwamini Mungu, na akahesabiwa kuwa na haki."

Nikasema, "Kweli."

Akasema, "Mtu anaweza kufanya nini zaidi ila kuamini?"

63 Nikasema, "Hivyo ndivyo tu mtu anaweza kufanya. Hivyo ndivyo tu anavyoweza kufanya leo, ni kuamwamini Mungu. Bali Mungu alimpa muhuri ya tohara," jambo tulilopitia jana usiku, "kama ishara kwamba Yeye alikuwa amekubali imani yake Kwake." Na, siku hizi, mpaka Mungu . . .

Unaamini katika Yeye unapomkubali kama Mwokozi Wako binafsi. Bali wakati Mungu anapokupa muhuri wa Roho Mtakatifu, Yeye amekutia muhuri hata kwenye kikomo chako cha Milele. Sasa ninyi Wabatisti chukueni jambo hilo, nami nitakubaliana nanyi juu ya usalama wa Milele. Naam, bwana. Kwa maana, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Hutiwi muhuri kwa kuamini ukitarajia, bali unatiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Waefeso 4:30, "Msimuhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwaye mumetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Huyo anakutia muhuri, wakati unapopata kibali kwa Mungu, Naye anakutia Muhuri kwa Roho Mtakatifu.

Hilo ni kweli, kwa kuwa Biblia ilisema: "Hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu."

64 Unasema, "Ninaamini hilo kwa maana mchungaji alisema hivyo." Yeye yuko sawa, bali hilo halikusaidii. "Ninaliamini kwa maana Neno linasema hivyo." Hiyo ni kweli, bali hilo si kwa ajili yako, hilo halikusaidii.

Njia pekee unayoweza kusema ya kwamba Yesu ni Kristo, ni wakati Roho Mtakatifu anapoingia ndani yako na kushuhudia, na kujishuhudia Mwenyewe, "Yeye ni Mwana wa Mungu!" Hivyo ndivyo tu unavyojua ufufuo, ni wakati Roho Mtakatifu anaposhuhudia. "Atakapokuja huyo Roho Mtakatifu, atanishuhudia Mimi, awaonyeshe mambo yajayo; awakumbushe mambo haya, niliyosema." Hutapata jambo hilo shuleni. Mnaona? Yeye atawakumbusha mambo haya.

65 Sasa tunataka kusoma mbele kidogo tu katika Andiko hili sasa. Yohana Mt. 14:12:

> *Amin, amin, nawaambieni, Yeye animiniye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko* . . .

Ambapo, tafsiri sahihi hapo ni "nyingi zaidi," kama ukitaka kulichunguza.

> . . .*kubwa kuliko hizo atazifanya, kwa kuwa mimi* ninaenda *kwa Baba.*

66 Kama Yeye alikwenda kwa Baba, Roho Mtakatifu angekuja. Hiyo ni kweli? Andiko lingine lilisema, "Nisipoenda, yule Msaidizi hatakuja. Bali nikienda, nitakuja tena na kuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu." Mnaona, ni Mungu pamoja nanyi. Juu yenu, kwanza; pamoja nanyi, katika Kristo; ndani yenu, katika Roho Mtakatifu. Mungu ndani yenu.

67 Naam, "Kazi nizifanyazo mimi ninyi nanyi mtazifanya," si kazi nyingine. Bali Mungu anataka kumleta Roho Mtakatifu, ndani yenu, kuendeleza kazi ile ile aliyokuwa akifanya katika Kristo.

Kazi hiyo haikuwa inahitajika sana katika siku za Luther. Hilo lilikuwa Kanisa la Mungu. Haikuwa. . .Ilihitajika zaidi kidogo katika siku za Wesley.

Kwa kuwa, "Ulimwengu," Biblia ilisema, "ungekuwa mnyonge zaidi, na wenye akili zaidi, na kuzidi kuwa mwovu zaidi wakati wote." Sisi tuna-. . .Ulimwengu unazidi kuwa mwovu wakati wo-. . .Tunajua jambo hilo. Mbona, mwanadamu anafanya mambo leo ambayo, miaka mia moja iliyopita usingefikiri kungekuwa na mwanadamu mkatili namna hiyo. "Wanazidi kuwa waovu daima, na walio waovu watazidi kufanya ukatili, daima," kasema Maandiko, "zaidi na zaidi."

68 Kwa hiyo, Roho Mtakatifu amekuwa akitenda kazi. Kulikuwa tu na uvuvio mmoja mdogo kwa Luther; uvuvio mdogo tu kwa Wesley; na uvuvio Wake mzito zaidi kwa Pentekoste; sasa ule uvuvio na Roho Mtakatifu vimekuwa kitu kile kile. Anaungana pamoja, akisababisha uvuvio ule ule wenye nguvu za Roho Mtakatifu kama Yeye alivyofanya kule nyuma, anadhihirisha kazi zile zile alizofanya kule nyuma, zinadhihirishwa moja kwa moja leo, jambo lile lile.

69 Angalia aliyosema Yesu. "Amini, amini nawaambieni, Mwana hawezi kufanya lo lote ila aone Baba akilifanya kwanza. Lile afanyalo Baba, Yeye humwonyesha Mwana. Baba anakaa ndani Yangu; Yeye hufanya hizo kazi." Mnaona?

70 Sasa angalieni, hapa kuna jambo lingine ningetaka kusema papa hapa. "Kama," Yesu alisema, "kama vile Baba alivyonipeleka Mimi. Kama," sasa angalia, "kama vile Baba alivyonipeleka, Mimi Nami nawapeleka." "Kama Baba . . . " Baba alimpelekaje? Baba, aliyempeleka, alishuka kutoka Mbinguni akakaa ndani Yake.

Alitoka akaenda. Akasema, "Daima Mimi hufanya yanayompendeza Baba Yangu." Mnaona? Yeye alienda kila mahali akifanya mambo ambayo Baba alikuwa anamwonyesha kufanya. "Mimi sifanyi neno ila Baba anionyeshe kwanza." Mungu aliyempeleka Yeye, alikuwa ndani Yake. "Basi kama vile Baba alivyonipeleka, jinsi Baba alivyonipeleka Mimi, Mimi Nami nawapeleka." Ni nini? Mungu ndani yako, akiendeleza (nini?) kazi zile zile, zile zile.

Yesu alisema, "Yule . . . yeye *aaminiye*, Yeye aliye Nami ndani yake, Roho Mtakatifu; yeye *aaminiye*, ambaye tayari ameshuhudia kufufuka Kwangu, anajua ya kwamba Mimi niko ndani Yake. Yeye aliye ndani Yangu; mkikaa ndani Yangu, maneno Yangu yanakaa ndani yenu."

71 Sasa unasema, "Mimi ninakaa katika Yesu; bali hakika siamini kuponya Kiungu." Hiyo inaonyesha Yeye hayumo mle.

72 "Ninamwamini Yesu; siamini Roho Mtakatifu katika siku hizi, si jinsi walivyokuwa Naye kule nyuma." Hilo linaonyesha Yeye hayumo mle.

73 Roho Mtakatifu atashuhudia kila Neno alilonena Yeye. Yeye si mdanganyifu. Hamwogopi mtu wala madhehebu yo yote. Haimbidi kumwondokea hata mtu. Yeye hunena, kisha anakaa nalo.

Kama watu walio wa hali ya juu, walioharibika, wenye elimu, ama kama tunavyoweza kuwaita, viongozi matajiri, iwapo hawataki kumpokea Yeye, "Mungu anaweza kutoka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Yeye atawachukua majambazi, wauza chang'aa, na cho chote, na kuwainua. Mungu anaweza kufanya jambo hilo, Naye analifanya. "Mungu anaweza kutoka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Mtu fulani atafanya jambo hilo, maana Yeye ni Mungu.

74 "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo," kwa maana mnaomba Neno Lake, na Neno Lake ni Uzima. Lineneni. Kama Mungu alisema jambo hilo, nawe una hakika alilisema, Roho Mtakatifu anashuhudia Neno hilo ni kweli, naam, haya basi, ndugu. Linene; Hilo hapo. "Uambie mlima huu, 'Ng'oka.' Usitie shaka moyoni mwako, amini ya kwamba yale umekwisha sema yatatimia." [Ndugu Branham

anapiga makofi mara tatu—Mh.] Si wewe unayesema, bali ni Baba anayekaa ndani yako; ndiye ananena. Si wewe unayenena na mlima ule, ni Baba aliye ndani yako, anayenena na mlima ule. Huna budi kung'oka. "Na mbingu zote na nchi zitapita," Yeye alisema, "lakini Roho Wangu hatapita . . . ama Neno Langu halitapita." Bila shaka, haliwezi kupita. Baba!

75 Naam, "Kazi nizifanyazo Mimi." Mungu yuko katika Kanisa Lake, kuendeleza kazi Zake. Hiyo ndiyo sababu Yeye alimtuma Roho Mtakatifu. Naam, Yeye alijua jambo hilo. Yeye, Yeye alijua haingekuwa, haingeweza kufanya namna hiyo, kwa hivyo ilikuwa ni vinginevyo, kwa hiyo ilimbidi kumtuma. Baba alimpeleka Mwana, akaweka yote yaliyo katika mwa- . . . Mwana ndani yako. Na kazi zile zile alizofanya, kazi zile zile sasa alizofanya Yesu, mtazifanya pia, enyi Kanisa.

Hivi usingetaka kufanya kazi za Mungu? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Yesu alisema, "Mkitaka kufanya kazi za Mungu, niamininі Mimi." Utamwaminije Yeye? Huwezi kufanya jambo hilo mpaka uwe na Roho Mtakatifu.

76 Maana, hakuna mtu anayeweza kusema Yeye ni Mwana wa Mungu; unasema kile mtu mwingine alichosema. "Biblia ilisema ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu; ninaamini Biblia." Sawa. "Biblia inasema ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu; ninaamini Biblia. Mchungaji anasema Yeye ni mwana wa Mungu; ninaamini mchungaji. Mama anasema Yeye ni Mwana wa Mungu; ninaamini Mama. Rafiki yangu anasema Yeye ni Mwana wa Mungu; ninaamini rakiki yangu."

Bali njia tu ninayoweza kusema Yeye ni Mwana wa Mungu, ni wakati Roho Mtakatifu anapoingia ndani na kujishuhudia Mwenyewe, ndipo ninajua Yeye ni Mwana wa Mungu. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara nne—Mh.] "Hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu 'Kristo,' ila kwa Roho Mtakatifu."

77 A-ha, hakuna mtu aliyenena kwa Roho wa Mungu aliyemwita Yesu aliyelaaniwa, ama kusema alikuwa kitu fulani siku hiyo na Yeye ni kitu kingine siku hizi. Jambo hilo linamfanya hafifu na mnyonge. La, bwana.

Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Roho ye yote wa kweli atashuhudia jambo hilo. Vema.

78 Naam, Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya," Yohana 14:12, naam, kazi zile zile.

"Loo," wao wanasema, "kanisa linafanya kazi kubwa zaidi siku hizi." Vipi?

Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi."

"Hizo," wao wanasema, "vema, tuna wamishenari kila mahali ulimwenguni, hizo ni kazi kubwa zaidi."

79 Bali Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi." Basi zifanyeni, zifanyeni kwanza, kisha mzungumze juu ya wamishenari.

80 Leo, akizungumza hapa wakati mdogo uliopita juu ya Waislamu, alisema, “Muhamadi amekufa.

“Hiyo ni kweli, yuko kaburini, lakini siku moja atafufuka.” Akasema, “Kama akifufuka kutoka kaburini, ulimwengu mzima utajua jambo hilo katika masaa ishirini na manne.” Akasema, “Ninyi watu mnasema Yesu amefufuka miaka elfu mbili, na hakuna theluthi moja ya watu wanaojua jambo hilo bado.”

Hiyo ni kwa sababu mlinena kiakili. Mlinena kutoka msimamo wa shule ama wa elimu.

Kama kanisa hili lote, lililo kuu la Mungu, tukihesabu Katoliki, Prostestanti, wote pamoja, walikuwa wamempokea Roho Mtakatifu, ulimwengu huu ungekuwa Ukristo mtupu; kusingekuwako na kitu kama Ukomunisti; kusingekuwa na kitu kama mizozo, wala uadui, wala uchoyo, wala chuki. Yesu angekuwa ameketi kwenye Kiti Chake cha Enzi, nasi tungekuwa tukitembea katika Paradiso ya Mungu, tukiwa na Uzima wa Milele, tukiishi milele; tayari tumefufuliwa katika mwili mpya, tukitembea kila mahali, bila kuzeeka, bila kuwa na mvi, bila kuwa wagonjwa, bila kuona njaa; tukitembea katika furaha ya Bwana, tukizungumza na wanyama. Na, loo, ni siku ya namna gani! Bali tumefanya kila kitu mbali na kile Yeye . . .

81 Yeye alisema, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili.” Injili inafanya nini? “Si Neno tu, bali kwa Nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu.” Kulifanya Neno la Mungu lidhihirike, ndiyo Injili.

82 Hamwezi kufanya jambo hilo. Sasa, Yesu alijua jambo hilo, ya kwamba ilimbidi kuishi katika Kanisa Lake.

Kwa hiyo, Yeye alijua tungekuwa na shule za kielimu. Nawe hutapata hili kamwe katika shule ya kielimu. Wao watalipinga. Kwa maana, yote wajuyo ni elimu ya mtu fulani mweruvu, baadhi ya kanuni za imani ama madhehebu wao wanataka ku—kuishi kwayo. Kwa hiyo wao—wao watakuinua katika hayo na kukufanya sehemu ya shirika hilo, na, ndugu, watakunukuulia baadhi ya vitu fulani kutoka kwa kanuni ya imani ambavyo vingeonekana kama kwamba ni kweli kabisa. “Kanisa kuu takatifu, lililo mama, lilistahimili mapigo mengi, lilistahimili kutwangwa kwingi.” Vivyo hivyo na ibilisi pia; amepigwa akatolewa kutoka kila mahali paliopo, karibu kila mahali, na angali anaendelea tu vile vile. Naam, bwana. Loo, wao watajaribu kuyanukuu haya.

83 Kwa hiyo Yesu alijua ya kwamba kungekuwako na mfumo mkuu wa kielimu kama tu uliokuweko katika siku Zake, kama vile kuoshwa kwa midumu na vikaango, na kuvalia nguo, na ukosi uliopinduliwa, na kila kitu walichofanya, mambo haya yote mbalimbali ambayo wangefanya. Yeye alijua wangefanya hayo, kwa hiyo akasema, “Hebu ngojeni tu kidogo. Sitawaacha

yatima, ninakuja tena kuwa pamoja nanyi. Kwa hiyo," Yeye akasema, "kazi nizifanyazo, ninyi nanyi mtazifanya."

84 Kusudi la kumtuma Roho Mtakatifu lilikuwa ili kwamba Mungu aendelee kupitia kundi la watu, kuendelea kumdhihirisha Mungu kwa ulimwengu. Hiyo ni kweli kabisa. Si kwa kanuni ya imani, si kwa madhehebu; bali kwa nguvu za kufufuka Kwake, kwa kulifanya neno Lake kuwa dhahiri; kwa kuchukua ahadi Yake, na kusimama upande wa walio wachache, na kumwamini Mungu; na kuangalia anga nyeusi zikirudi nyuma, na Nguvu za Mungu zikiingia na kutawala. Amina. Hivyo ndivyo anavyotaka Yeye. Hilo ndilo kusudi la kutumwa kwa Roho Mtakatifu. Hilo ndilo kusudi la Yeye kumtuma. Tunajua Yeye ni nini sasa, na hiyo ndiyo sababu Yeye alimtuma.

85 Kwa hiyo, hakuna damu nyingine ingeweza kuwatakasa watu. Nisingeweza kuwatakasa ninyi, wala nanyi msingeweza kunitakasa mimi, maana sote wawili tulizaliwa kwa njia ya kujuana kimwili. Bali Yesu alizaliwa bila kujuana kimwili, hiyo ni kweli, kwa hiyo Damu Yake ilikuwa yenye kutakasa. Ndipo Mungu akashuka, akafanyiwa mwili, akaishi ndani yake, akamwaga Damu ile kwa ajili ya kuutakasa huu, jambo ambalo liliondoa kabisa hatia ya dhambi na aibu. Ndipo, kwa imani, kwa kuamini jambo Hilo, Mungu anashuka moja kwa moja na kuingia katika mwili huo wa binadamu, kwa kutakaswa na Damu hiyo, kunamfanya Mzao wa Ibrahimu, kwa imani.

86 Kuamini ya kwamba Damu hiyo ingekuja, Damu hiyo iliyo safi ambayo ingekuwa muujiza kama ile damu Yake, alienda kule baada ya "kuwa kama aliyekufa." Akamwamini Mungu kwa miaka ishirini na mitano, naye akiwa na umri wa miaka sabini na mitano, akaamini mpaka alipokuwa na miaka mia moja. Naye Sara, sitini na mitano, akaamini hata alipokuwa na umri wa miaka tisini. "Naye alikuwa kama aliyekufa."

Kisha Mungu akasema, "Ili kwamba watu wahakikishe hawatalikosa, mpandishe humu kilimani ukamtoe dhabihu."

87 Akawaambia watumishi wake, "Ninyi simameni hapa pamoja na nyumbu mkangojee. Mimi na mwanangu tutaenda kule tukaabudu, nami na mwangangu tutarudi!" Loo, atafanyaje jambo hilo?

Ibrahimu akasema, "Nilimpokea kama mmoja aliyefufuka katika wafu. Nami najua ya kwamba Yeye aliyemtoa kwangu, kama mmoja aliyefufuka katika wafu, anaweza kumfufua katika wafu kama tu nikitimiza Neno Lake. Kutimiza, nikitimiza Neno Lake; Yeye anaweza kumfufua katika wafu."

88 Akinena kikamilifu kumhusu Kristo. Huyo hapo. Basi kupitia kwa chembechembe hiyo ya Damu akatoka Roho Mtakatifu, ambaye alikuwa amejizungushia mwili ulioitwa Yesu. Damu hiyo ilitakasa njia, kwa imani, kuwaita

waliokombolewa, ama Wateule wa Mungu. Ndipo wakati umeikubali Hiyo, na Roho Mtakatifu ametoa uchoyo wote kutoka kwako, Yeye huingia moja kwa moja ndani, Mungu Mwenyewe, kufanya mapenzi Yake.

89 Huku chini, huyo bosi mbaya mwenye kisirani; na huyu *wa kale fulani* mwingine huku anafanya *kadha wa kadha*; na maskini jamaa *huyu* anazungumza habari Zake, dhidi yake. Mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu atalibariki jambo hilo moja kwa moja. Amina.

90 "Nao wakatambua. Walikuwa wasio na elimu wala maarifa, bali wao walitambua walikuwa pamoja na Yesu." Hilo ndilo kusudi la kuja kwa Roho Mtakatifu.

91 Maskini mzee mfua samaki asingeweza kuandika jina lake. Bali alisimama pale akasema, "Tutamwamini nani, mwanadamu ama Mungu?" Amina. [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] "Na ijulikane kwenu, tungali tutahubiri katika Jina la Yesu." Jamani, ni ujasiri wa jinsi gani! Yeye alijua a—alikuwa na makao kule ng'ambo. Hiyo ni kweli. Alikuwa msafiri na mgeni hapa. Alikuwa akiutafuta Mji ujao.

Huyo kuhani mnafiki alimaanisha nini kwake? Yeye alikuwa chini ya utawala wa Mungu wa Mbinguni, aliyemfufua Mwanawe, Kristo Yesu, na kumjaza na Roho wa Mungu aliyeziumba mbingu na nchi. Haya basi. Yeye hakushtushwa naye. La, bwana. Mauti . . .

92 Mbona, walipomtoa maskini Stefano kule nje, na kusema, "Ghairi jambo hilo!"

Yeye alisema, "Enyi wenye shingo gumu, na msiotahiriwa mioyoni wala maskioni, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu. Kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo."

Wao wakasema, "Tutakupiga hata ufe."

Akasema, "Msingeweza kufanya hivyo . . .?. . . "

"Tutakuonyesha kama tutafanya hivyo ama la!" Ndipo wakanyakua mawe makubwa wakaanza kumtwanga kichwani.

93 Akatazama juu, akasema, "Naona Mbingu zimefunguka. Naona ngazi ikishuka. Namwona Yesu amesimama mkono wa kuume wa Utukufu Wake!" Wala Biblia haikusema alikufa; alilala. Loo, jamani! Naweza kumwona Malaika akishuka, akumchukua, na kumpembeza kama mtoto, mama fulani, hata akalala. Loo, jamani! Hakika.

94 Hilo ndilo kusudi la Roho Mtakatifu. Na hilo ndilo kusudi la Mungu kumpeleka Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu alikuja kukupa Nguvu. Nina Maandiko mengine hapa. Hebu kidogo. Roho Mtakatifu alikuja kukupa Nguvu. Mimi—mimi si-. . . Mnaweza kupata hili; Nimechelewa sana, usiku huu.

Kukupa Nguvu, Nguvu katika maombi!

95 Mchukue mtu aliyeishi maisha mazuri, bali daima wanashindwa. "Loo, nakwambia . . . " Mtu mzuri. "Loo, hakika, nampenda Bwana, Ndugu Branham." Daima wanashindwa; hawapati ombi lililojibiwa.

Mjaze maskini mwanamke huyo na Roho Mtakatifu wakati mmoja, angalia kitakachotukia. Anapoenda mbele za Mungu, yeye hashindwi. Anakuja kwa ujasiri kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, akiamini. Anayo haki kwa maana yeye ni binti wa Mungu, kwa Kuzaliwa.

Mchukue maskini mwanamume huyo, mwoga sana, bosi anamsukuma kila mahali. Kasema, "Ngoja kidogo hapa sasa." Kitu fulani kilibadilika, mnaona, yeye yuna Roho Mtakatifu. Yeye anakupa Nguvu. Maisha yako yamejaa Nguvu.

Anakupa Nguvu katika mazungumzo.

96 Mbona, jamani, watu hao hawakuogopa, wakisimama kule nje; Petro, Yakobo, na Yohana, Luka, na hao wengine wote. Tayari walikuwa wameingia kwenye chumba cha juu, wakisema, "Loo, hatuwezi kunena tena. Wao, angalieni kule, Yule pale nje Dk. *Fulani na fulani*. Yule pale Rabi *Fulani na fulani*. Mwajua, alikuwa na digrii nne za chuoni; tutawezaje kamwe kumkabili? Petro akasema, "Loo, nakumbuka nikimuuzia mtu yule samaki siku moja. Yeye, yeye alinena, na hata sikujua alilokuwa anazungumzia. Loo, ninsingeweza kumkabili." Lakini nini . . .

"Tufanye nini, ndugu?"

"Yeye alisema, 'Ngojeni.'"

"Vema, tayari tumekuwa hapa siku nne."

"Endeleeni tu kungojea."

"Mpaka lini?"

"Hata."

"Vema, hivi Yeye alisema itakuwa kwenye siku ya tano?"

"Yeye hakusema ni muda gani. Alisema, 'Hata.'"

Vema, waliendelea tu kungojea. "Muda gani?" "Hata!" Siku nane zikapita. "Hata." Siku tisa zikapita. "Hata."

> Hatimaye *siku ya Pentekoste ilipotimia, walikuwako wote* mahali pamoja, wakiwa na moyo mmoja.

97 Mungu alikwisha kuwa juu yao, katika Wingu la moto; Mungu alikuwa tayari ametembea pamoja nao, duniani; sasa kitu kingine kilikuwa kitukie. Kitu fulani kinakaribia kutukia.

> . . . *wote walikuwa* mahali pamoja, na moyo mmoja.

> *kukaja ghafula kutoka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukakijaza chumba chote walichokuwa wameketi.*

> . . . *ndimi zilizogawanyikana* . . . zikakaa juu yao.

*Zilizogawanyikana* ni nini? "kugawanyika." Kama kugugumiza, Umeshamsikia mtu ye yote akigugumiza maneno? Wao wanafanya, "Ah, ah, ah, ama, ah-ah," mnaona, hawawezi kusema kitu. "Kugawanyikana, kuachana." Kama kwato *mbili*, inamaanisha kitu "kilichopasuliwa, kilichotenganishwa." Hawakuwa wakizungumza. Hawakuwa wakipayuka. Hawakuwa wakifanya kitu ila ni kupiga makelele tu.

> *Ndimi zilizogawanyikana* zikakaa juu yao, kana kwamba ilikuwa ni moto. (Loo, wasingweza kujizuia.)
>
> *Wote Wakajazwa Roho Mtakatifu* . . . Whiu!

98 Ndipo kukatendeka nini? Wakatoka wakaenda mitaani. "Yuko wapi yule Rabi Jones? Jamaa huyo yuko wapi? Liko wapi lile jitu la kiakili?"

"Mungu alikuwa juu yetu, pamoja na Musa, katika kijiti kilichowaka moto; Yeye alitulisha mana, itokayo Juu. Alitembea pamoja nasi kwa muda wa miaka mitatu na sita . . . miaka mitatu na miezi sita, hapa duniani. Bali sasa Yeye yumo ndani yangu. Si mimi ninayezungumza; ni Yeye. Ninajua Yeye ni nani, ninajua mimi ni nani. Mimi sipo tena; Yeye yupo."

> Mleteni hapa! *Enyi waume wa* Israeli, nanyi *mnaokaa* katika Yuda, *lijueni jambo hili—lijueni jambo hili, mkasikilize* sauti *yangu*, enyi wahubiri wote na marabi.

Whiu! Jamani! Nguvu za kunena! Loo! "Watu hawa hawakulewa!" Akiwatetea hao walio katika uchache, mia moja ishirini, dhidi ya elfu kumi au zaidi.

> . . . *watu hawa hawakulewa* kama mnavyodhania, *kwa maana ni saa tatu ya mchana*.
>
> Mimi ni mhubiri wa Injili Yote. *Lakini jambo hili ni lile lililonenwa* na *nabii Yoeli,*
>
> *Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia* (whiu) *watu wote Roho Yangu, na wana wenu* . . . Mmemwona Mariamu kule nje akicheza katika Roho, akinena kwa lugha na kupiga makelele? . . . *nitawamwagia watu wote* . . .
>
> . . . *juu* ya watumishi Wangu wanawake nitaimwaga . . . *Roho Yangu* . . .

[Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu.]

> . . . Nitaonyesha ishara katika mbingu *juu, na* . . . *katika nchi chini*, nguzo za *moto na* mivuke ya *moshi*.

Mungu ndani ya watu Wake wakati huo. Amina.

"Vema sasa, ulikuwa na digrii gani?" Wapi, ulitoka kwenye shule gani?"

99 "Hilo halileti tofauti yo yote sasa hivi?" Loo, akaanza kuyamwaga Maandiko.

> "Daudi alimwona Yeye hapo awali! . . . '*Bwana mbele yangu sikuzote* . . . mimi *nisitikisike*.
>
> . . . tena *moyo wangu* ulipendezwa, kwa sababu . . . *ulimi wangu* ulifurahishwa;
>
> . . . hataiacha *roho yangu katika kuzimu; wala* hatamtoa *Mtakatifu* wake *aone uharibifu*.'
>
> . . . *mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi . . . alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu . . . leo*.

Bali kwa kuwa nabii . . . , alitangulia kuona kule kuja kwa yule Mwenye Haki.

> Na ijulikane kwenu, *ya kwamba Mungu amemfanya Yesu* yuyu *huyu mliyemsulubisha* kwa mikono miovu *kuwa Bwana na Kristo!* Amina!

100 "Waume na ndugu zetu, tufanyeje tupate kuokolewa?"

> . . . kasema, "*Tubuni*, kila mmoja wenu, *makabatizwe katika jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*
>
> *Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie*. Amina.

101 Mradi tu Mungu anao watu, Mungu analo Kanisa, Mungu anaye Roho Mtakatifu akipiga hatua pamoja Nalo. Hilo ndilo kusudi la Mungu kumtoa Roho Mtakatifu. Wenye akili watainuka; daima wameinuka. Bali Mungu ana walio wachache mahali fulani. Mungu analo Kanisa dogo litakalopiga hatua moja kwa moja na ubatizo wa Roho Mtakatifu, kudai ile Nuru. Nao watakuwa ndio, kwa ushuhuda wao, watakaouhukumu ulimwengu.

Hivi Biblia haisemi ya kwamba Yesu alisema, "Heri wenye moyo msafi; watamwona Mungu"? Na hivi si inasema, ya kwamba, wenye haki, watakatifu, wataihukumu dunia"? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Hakika.

Ushuhuda wako leo utaleta hukumu juu ya jiji hili. Ushuhuda wetu wa ubatizo wa Roho Mtakatifu na Nguvu za Mungu, maisha matakatifu, utaleta hukumu juu ya jiji hili. Wakati hili . . .

102 Hao walio wa kwanza watakuwa wa mwisho; hao walio wa mwisho watakuwa wa kwanza." Sitajua kitu juu ya Sankey na Moody, katika ufufuo wao. Wao hawatajua kitu kunihusu mimi, katika huu. Bali nitasimama katika huu, kutoa ushuhuda; nawe pia.

Na kupitia jambo hilo, kwa kutawanya Nuru zenu, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kwa maisha mliyoishi, na mambo ambayo Mungu amefanya kuthibitisha ya kwamba anatenda

kazi hapa; na pamoja na wenye akili wao, wakaliondokea Hilo; wao watahukumiwa na watakatifu. Wao tayari wamehukumiwa. Tayari wamelipita. Loo, jamani!

103 Nilikuwa nikizungumza juu ya Nguvu za maombi, Nguvu za kuzungumza, Nguvu za maisha matakatifu. Amina. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu atafanya.

104 Baadhi yenu watu mkitembea, mkisema, "Vema, siwezi kuacha kunywa pombe. Siwezi kuacha kufanya jambo *hili*."

Roho Mtakatifu anakuja kuishi ndani yenu, kuzifanya hizi "siwezi" zote zikuondokee. Hiyo ni kweli. Kuwafanya wanawake waache kukata nywele zao, kuwafanya waache kuvaa kaptura na suruali ndefu. Hapana udhuru. Kuwafanya waache kupayukapayuka. Loo, naam, hilo ndilo kusudi lake, kukufanyia maisha matakatifu. Atafuata maagizo ya Biblia kila wakati.

105 Mwanamke anasema, "Ni joto mno; sina budi kuvaa hizi. Ninaumwa na kichwa nikiacha nywele zangu zikue."

Bali hakuna udhuru kwa Roho Mtakatifu. Yuko pale kuifanya hivyo. Atalifuata neno kabisa! Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu atafanya.

Atakufanya wewe mwanamume kugeuza kichwa chako mbali na wanawake hao walio nusu uchi, na kuacha kuwatamani, nao ni wafuasi wa kanisa. Hivyo ndivyo atakavyofanya.

106 Ni kukufanya uache kuvute sigara na kunywa pombe, na kuwa . . . kutaka kuwa mtu mkubwa. Atakuondolea jambo hilo. Atakufanya mnyenyekevu ukifanya hivyo. Hilo ndilo kusudi la Roho Mtakatifu. Ni kwa ajili ya maisha matakatifu. Hiyo ni kweli. Kukufanya uache kupiga domo. Kukufanya uache kucheza karata, kusengenyana, na mambo haya yote mengine unayofanya pembeni.

Atakufanya uache kufanya yasiyofaa jinsi unavyofanya, kuishi ukiwa si mwaminifu kwa mke wako. Hivyo ndivyo atakavyofanya. Hiyo ni kweli. Atakufanya uache kutaka kumwoa mke wa mtu mwingine. Hiyo ni kweli kabisa.

Hivyo ndivyo alivyo Yeye. Atakufanya uishi maisha matakatifu. Hilo ndilo kusudi la Nguvu za Roho Mtakatifu, "kuyafikiria mambo yaliyo Juu," ambako Mungu anasimama kwenye . . . ? . . . Nia ya Kristo ndani yako. Huwezi kujizuia kuona mambo hayo; unapoyaangalia, unageuza kichwa chako. Hiyo ni kweli. Ni kukufanya.

107 Unasema, "Siwezi kufanya jambo hilo. Loo, siwezi kulifanya." Hakika, *huwezi*.

Lakini Roho Mtakatifu anakuja kwa kusudi hilo. Hivyo ndivyo alivyofanya. Alikuja kuzitoa kwako, hizo tabia za kale zote na mambo unayofanya.

Huko kusengenyana kwa kale, kujitenga mwenyewe, ukisema, “Mungu abarikiwe, mie ni Mmethodisti, sitajihusisha kamwe na hilo kundi la watakatifu wanaojifingirisha.” Roho Mtakatifu huja kuondoa kitu hicho ndani yako.

108 “Mie ni Mbatisti. Mie ni Mpresbiteri. Siwezi kwenda kwa maskini kundi lile la watakatifu wanaojifingirisha.” Roho Mtakatifu huja kutoa ugumu huo wote kutoka kwako. Hivyo ndivyo alivyofanya. Anakuosha kwa Damu; anakunyosha. Hivyo ndivyo anavyokuja kufanya.

Anakuja kukunyosha. Yeye alisema, “kufanya mahali palipopindika panyoke.” Hivyo ndivyo alivyokuja kufanya; kupanyosha. “Kushusha mahali palipoinuka; kuifanya milima yote ionekane kana kwamba yote inacheza kama kondoo wadogo, na majani yote yanakupigia makofi, wewe.” [Ndugu Branham anapiga makofi mara nne—Mh.] Ndege wanaimba tofauti. Kengere za shangwe zinalia. Hakuna udhuru. Hivyo ndivyo Huyo anavyokuja kufanya. Hilo ndilo kusudi la Mungu kumtuma Roho Mtakatifu, ili kwamba uweze kufanya mambo haya, ili kwamba upate kufanya kazi—kumwandama Yeye.

109 Sasa sitaki kuwaudhi, bali niliwaambia niko hapa kwa uaminifu mwingi mno. Kusudi nisiwafinye, mara kwa mara ninaruka mstari mmoja mahali fulani; na kukaa tu na ile Kweli, lakini nikidumu pale na kulifanya kwa namna fulani hata lisiwafinye mno.

110 Bali nataka kuwaambieni jambo fulani. Kama Biblia inasema ni vibaya kwa mwanamke kukata nywele zake, nawe unasema una Roho Mtakatifu halafu ukate nywele zako, nashaangaa kama unaye. Usikasirike sana; kama ukikasirika, hilo bado linaonyesha kuna alama nyingine dhidi yako.

111 Kama Biblia inasema si halali kwa mwanamke kuvaa vasi linalompasa mwanamume, nawe unavaa maskini ovaroli hizi za kale na suruali ndefu huku nje barabarani, ninyi wanawake wakubwa! Nadhani kwa mtoto mchanga ingekuwa sa-. . . kitu, kwamba wao wanacheza na wavulana wadogo na kadhalika. Lakini, angalieni, wakati ninyi—wakati ninyi wanawake mliokomaa wenye umri wa miaka kumi na mitano, kumi na sita, kumi na minane, kufikia nyanya, huku nje barabarani! Na Biblia ilisema, “Ni chukizo mbele za Mungu,” kwa mwanamke kuvaa vitu hivyo. Nanyi mnavivaa hata hivyo, kisha mseme mna Roho Mtakatifu? Sijui wakati mwingine. Roho Mtakatifu atalifuata Neno la Mungu neno kwa neno.

Na mhubiri nyuma ya mimbara, asiye na neema ya kutosha kuhubiri jambo Hilo, nashuku kama yeye anaye Huyo. Hiyo ni kweli kabisa! Vema, hilo ndilo kusudi la Roho Mtakatifu.

112 Atampa mhubiri upako. Atalipa hilo kundi utakatifu. Ataliweka Kanisa katika utaratibu. Ataleta umoja wa roho.

Atatuunganisha pamoja na Nguvu. Ata-. . . tuunganisha pamoja kwa upendo, upendano wa ndugu.

Sijali kama wewe ni Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteri, Mluteri, cho chote ulicho, kama sote tumebatizwa katika Roho Mtakatifu mmoja kuwa Mwili mmoja, na kuwa washiriki wa Mwili wa Yesu Kristo. Hakuna. . . Hakuna kilichoko, hakuna kijacho; njaa, kufa kwa njaa; hakuna kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu, upendo wa Kristo, "upendo wa Mungu ulio katika Kristo," kwa maana tumezaliwa kwa Roho Wake, tukaoshwa kwa Damu Yake. Sisi ni kiumbe kipya. Hivyo ndivyo Mungu alivyokuja kufanya. Hilo ndilo kusudi la Roho Mtakatifu. Naam, bwana. Hivyo ndivyo.

113 Naam, enyi watu, niangalieni usoni. Mikono mingi iliinuliwa, kwamba mlikuwa na Roho Mtakatifu; mnaona, hakika, ilikuwa mingi. Loo, sasa, nitaruka kidogo tu hapa. Haya yananaswa. Lakini tutapata mengi yake kesho usiku.

Kama ukisema unaye Huyo, nawe una hatia ya mambo haya, sijui ni kitu gani kinachokuongoza. Mungu hatakuongoza nje ya Neno kamwe. Yeye atakudumisha kwenye Neno, maana hizo ndizo sheria za Mungu Mwenyewe, kwa Kanisa Lake, kwa ajili ya watu Wake, kwa ajili ya wanawake, kwa ajili ya wanaume.

114 "Vema," unasema, "Hainidhuru kufanya jambo *hili* wala *lile*." Haikudhuru? Neno linasema inakudhuru.

Na iwapo Roho Mtakatifu yumo ndani yako, atakuongoza moja kwa moja kwenye Neno. Hakutakuwa na udhuru. Mungu hafanyi mabadiliko wala udhuru. Yeye anatia alama nawe unaifuata. Hivyo tu. Hivyo ndivyo ilivyo kwa kila mtu. Unakuja kwa njia iyo hiyo.

115 Petro alisema, "Tubuni kila mmoja wenu; mkabatizwa, kila mmoja wenu, katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, kisha mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Mnaona? Naam. Hatuna budi kufikia mstari huo.

116 Sasa sikusudii kuwaudhi; nawapenda mno. Lakini, ndugu, dada, hivi unatambua, kile. . . ya kwamba ninajua ya kwamba sina budi kusimama katika siku za mwisho kwenye ule ufufuo, pamoja na kizazi hiki cha watu, na kutoa hesabu kwa ajili ya Neno hili? Na Roho Mtakatifu akionyesha jambo hili, nami nikilihubiri huko ng'ambo, utasimama wapi? Utaepukaje jambo hilo? Huwezi kufanya jambo hilo, rafiki. Usifanye hivyo. Sasa komesha jambo hilo. Lo lote unalofanya ambalo ni kosa, likomeshe.

Unasema, "Siwezi."

Basi huna "Mweza" ndani yako bado. Roho Mtakatifu ajapo, anakupa Nguvu juu ya ulimwengu. Na kama wewe. . . Sikiliza alilosema Yeye. "Ukiupenda ulimwengu ama mambo ya ulimwengu, ni kwa sababu kumpenda Mungu hakumo ndani

yako." Basi, hakuna udhuru. Yeye analifanya wazi, nasi hatuna budi kufikia kiwango hicho.

117 Najua mnafikiri mimi ni mbaya sana. Bali mimi nimejaa vibaya sana sasa hivi. Mnaona? Sikilizeni. Hiyo ni kweli. Basi, njoo Kwake, ndugu, dada.

118 Usiache baadhi ya vyuo hivi vya elimu karibu na hapa vikwambie, "Loo, huo ni upuzi wa mzee wa mtindo wa kale."

Kama ni upuzi wa mzee wa mtindo wa kale, basi Mungu ni mzee wa mtindo wa kale. Na iwapo Mungu ni mzee wa mtindo wa kale, basi mimi ndivyo nilivyo, pia. Amina. Ninataka kuwa kama Yeye. Kwa nini? Roho Wake yuko ndani yangu, anayeona njaa na kiu, akiita kila kitu kinachopingana na Neno . . .

119 Kama watu wakisema, "Ni sawa kwa, loo, kama mtu akicheza karata kidogo kwa kujiburudisha, na kuchezea hela moja ama mbili. Ni sawa." Mungu anasema si sawa.

120 "Loo, kama ukinywa pombe nzuri ya umma, ulewe tu kidogo mara kwa mara."

Lakini Mungu alisema, "Ole wake!"

121 "Loo," unasema, "ni sawa, Ndugu Branham. Ni—ni—ninakata nywele zangu kwa sababu halisi. Mwanamke, wajua, wanawake wengine wanafanya jambo hilo." Sijali wanawake wengine wanafanya nini. Wao sio mfano wako wala sio bosi wako. Kama una Roho Mtakatifu ndani yako, utafuata maagizo Yake haidhuru watu wanasema nini juu yako.

122 "Vema, Ndugu Branham, ni joto sana, nami sina budi kuvaa maskini nguo *fulani* hizi." Jehanamu ina joto zaidi, dada mpendwa. Hebu nikwambie jambo hilo. Wa-wala usifanye hivyo. Kumbuka jambo hilo tu.

123 Naye Roho Mtakatifu daima atakuongoza kwenye ile Kweli, na Kweli Yake ni Neno. "Neno Langu ni Kweli. Neno la kila mtu na liwe uongo, lakini Langu liwe kweli."

Basi wazia tu, "chukizo." Ungewazia?

124 Hili ni Neno baya sana kwa mhudumu kusema, bali nilienda kwenye misala ya mahali ambako ingenini hii tu . . . Ingekupasa karibu utoke mle, ilikuwa tu nini hii sana . . . Na vitu vichafu kutani. Nikawaza, "Watu wanawezaje kamwe kuwa duni namna hii?" Na harufu mbaya! Basi ninapoingia mahali pale, mara nyingi nimewazia, "Harufu mbaya jinsi gani!" Ninge- . . . mle ndani, ningeshikilia pua langu namna *hii*, kusafisha mikono yangu. Ningeogopa ya kwamba nitakaposhika kinundu cha mlango, tena, kungekuwako na viini vya kisonono na kadhalika. Ndipo nikawaza, "Loo!"

125 Siku moja, huku nimesimama kwenye uwanja wa ndege, moja ya mahali nilipoingia, ama ilikuwa ni kwenye reli, niliingia mle. Nikawaza, "Loo, rehema!"

126 Ndipo Kitu Fulani kikaniambia, "Hivyo ndivyo ulimwengu unavyonuka kwa Mungu. Ni chukizo."

127 Nikawaza, nilipomwona mwanamke akitembea mitaani, huku anajimudu namna hiyo, amevalia nguo za mwanamume, hivyo ndivyo inavyoonekana kwa Mungu. Ni chukizo, kitu ambacho ni kichafu na kinanuka, mbele za Mungu. Hata hivyo, ataenda kanisani Jumapili, na kujipodoa.

Mwanamume fulani atashuka aende kule, na kunywa, na kudanganya, na kupenda pesa, na kumdanganya jirani wake, na cho chote kile kupata fedha kidogo zaidi; na kufanya mambo haya, na kucheza kamari, na kuvuta sigara, na kunywa pombe, na kudanganya; kisha ataenda kanisani kutoa ushuhuda. Chukizo! uchafu! Hilo ni kanisa la kielimu.

128 Kasema, "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa." Naam, na hawana budi kuliacha kanisa litoke nje, dakika kumi na tano, ili mashemasi wote na hao wote waweze kuvuta sigara, na mchungaji, pia, kabla hamjarudi kuwa na kanisa. Niambieni? Jitengeni na kila jambo lililo chafu!

129 "Kuuchafua mwili; nitauangamiza." Mungu alisema angefanya jambo hilo. Na siku hizi, juu ya kansa, inasababisha asilimia tisini na kitu ya mauti, ya kansa ya koo na ya mapafu, inasababishwa na kuvuta sigara. "Ukiuchafua mwili; nitauangamiza." Lakini wao wanaelekea jehanamu sana, wakifingirika namna hiyo, hawajui.

Na mhubiri fulani akisimama mimbarani huku ana digrii nne, kutoka chuoni, mwenyewe akivuta sigara. Hebu nikwambie jambo fulani, ndugu. Roho Mtakatifu alitumwa kuwaita wanaume na wanawake kutoka kwenye kitu hicho. Jitenge wewe mwenyewe!

Neno *kanisa* linamaanisha "kujitenga." "Tokeni kati yao," ilisema Biblia. "Msiguse vitu vyao vilivyo vichafu, Nami nitawapokea; nanyi mtakuwa wana na binti Zangu, Nami nitakuwa Mungu kwenu." Loo, jamani! Sitaki kuwa mbaya, bali ninataka kuwa mwaminifu na mkweli. Naam, bwana! Loo, ni jambo la kuchukiza namna gani!

130 Enyi wanaume na wanawake, tunasimama wapi leo? Tuko wapi? Hebu tukome.

131 Juzijuzi usiku, kwenye kiti kidogo cha kale mle chumbani, (nami sina budi kufunga), kiti kidogo cha kale cha watu wawili. Baada ya kuomba kwa muda wa siku tatu ama nne, kwa hiyo nikafikia mahali, huku ninazunguka, na kufikiri, "Ee Mungu," nami nikafikia mahali fulani hata sikujua la kufanya. Nikasema, "Mungu, tumefikia mwisho wa barabara. Nami ninatambua ya kwamba sikujali. Nimepata simu za kuendelea, na nilikuwa mchofu, nami nisingefanya jambo hilo." Wakati huo nikawaza ningeweza kumwona Bwana wangu akiyumbayumba gizani kule, alipokuwa mchofu sana ilikuwa vigumu Kwake

kuinua mguu mmoja baada ya mwingine, bali hakuwa nini hii sana . . . Alisimama kwa ajili ya yule mwanamke wa Naini, kwa ajili ya yule mvulana aliyeletwa kule nje akiwa amekufa; hata Yeye angeenda kule na kugusa kile kitanda, na kutumia nguvu ndogo iliyokuwa ndani Yake kumfufua mvulana yule. "Vema, mimi nilipataje kuchoka? Kuna nini kwangu, Bwana?" Hapa ninafikiri, 'Vema, ninakuwa mzee. Si—siwezi kufanya jambo hilo.'"

132 Kulikuweko na Musa, Mungu yule yule ninayemtumikia, alisimama pale, akiwa na umri wa miaka mia moja na ishirini.

Kulikuweko na Kalebu, alisimama akiwa na umri wa miaka tisini, akiwa na upanga mkononi mwake, na kusema, "Yoshua, aliuweka upanga huu mkononi mwangu, miaka arobaini iliyopita." Alikuwa na umri wa miaka themanini wakati huo. Kasema, "Mimi ni mzima leo kama nilivyokuwa wakati ule." Amina!

Nikasema, "Mungu, nirehemu mimi."

133 Nikasema, "Vema, angalia hapa, mimi daima . . . " Ndipo nikamshika mke wangu (kule nyuma) mkono, juu ya Biblia hii na Biblia yake ndogo, nikasema, "Mpenzi, nimekuwa kinyume mno. Roho Mtakatifu ananihukumu ndani yangu." Nikasema, "Ninafikiria juu ya kindi wale kule ng'ambo. Ninafikiria juu ya Hattie Wright kule nyuma, na hao wavulana wadogo. Ninafikiria juu ya yale Mungu aliyofanya, akionyesha ya kwamba Yeye alikuwa Mungu, anayeweza kuumba." Haleluya!

Nikawaza, "Yeye amekwisha kuniambia jambo hilo, miaka kadha iliyopita, 'Sitakuacha. Sitakupungukia. Hakuna mtu atakayesimama mbele zako, siku zote za maisha yako. Nitakuwa pamoja nawe. Na kutoka mkono huu wa kupambanua, itakuja mpaka utajua siri ya moyo. Baada ha hayo, itainuka juu zaidi na zaidi!' Basi baada ya jambo hilo, ilithibitiska kikamilifu, kila mahali ulimwenguni. Hii hapa inakuja, huduma hii nyingine iliyo kuu sana kuliko hiyo."

Nikasema, "Mpenzi, ninaushika mkono wako. Kwa msaada wa Mungu na neema ya Mungu, usiniache niwe kinyume tena. Hebu niende zangu kwenye ufufuo huu hapa nikahubiri kuliko nilivyopata kuhubiri hapo awali. Hebu niende hapa, nikajitakase mwenyewe kwanza, na kuwafanyia watu njia; ili kwamba dhambi zangu mwenyewe, kutojali kwangu mwenyewe kuwe chini ya ile Damu, kupungukiwa kwangu mwenyewe kuwe chini ya ile Damu, nipate kutoka nje na kusema, 'Nifuateni, enyi watu!'" Hiyo ni kweli.

Ninachukia kumwona jamaa fulani akisema, "Wewe nenda ukafanye jambo hilo." Ninapenda kumwona mtu fulani atakayeongoza njia kufanya jambo hilo. Naam, bwana.

134 Hapa wakati fulani uliopita, tulikuwa na moto mjini hapa, Kampuni ya Mafuta ya Pfau ilishika moto. Walikuwa na Idara

ya Zimamoto ya Jeffersonville kule chini. Na rafiki yangu, mtu mzuri, hakuzoea mioto mikubwa namna hiyo, alikuwa anatembea kule, akisema, "Rusheni maji madogo *huku*, enyi wavulana. Rusheni maji madogo upande *huu*."

Huyu hapa maskini wa Clarksville kule juu, "ding, ding, ding, ding," wakakimbia kule juu. Naye akasema, kiongozi wa zimamoto akaruka, kasema, "Rusheni maji madogo *hapa* chini. Vunjeni dirisha hili *hapa*. Rusheni maji madogo *pale*."

135 Bali kutoka ng'ambo ya mto wakaja zimamoto waliofunzwa kutoka Luoisville. Mara ile kulabu kubwa na ngazi iliposimamishwa yule kiongozi alikuwa mwishoni mwa ile ngazi. Ile ngazi iliposimamishwa, alikuwa anaongoza. Akatupa shoka lake kabla hajafika kule, akalivunja dirisha, akasema, "Njoni, enyi vijana!" Jambo ndilo hilo. Ule moto ukazimika katika dakika chache.

Si, "Rusheni maji kidogo *hapa*. Rusheni maji kidogo *pale*." Inanikumbusha, baadhi ya wahubiri hawa wenye elimu.

136 Njoni! Haya twende! Ninajua ni kweli. Nimeonja na kuona. Utukufu! Roho Mtakatifu ni kweli. Mungu yu mwema. Msijaribu *hapa*, mjaribu *pale*; haya twende Kwake! Yeye yuko hapa. Ni kwa ajili yako. Mungu alitoa nguvu Zake kwa Kanisa Lake. Si rusha haya *hapa*, na uyarushe nje; hutafanikiwa kufanya lo lote. Ongoza! Amina. A-ha! Whiu!

Huwezi kuonea kwayo tena. [Ndugu Branham anatoa miwani yake ya kusoma—Mh.]

137 Amina! Tutafanya nini? Kila mtu aliyeketi hapa amejazwa kitu fulani.

Kisha nitafunga; huenda ikanilazimu kufunga, baada ya jambo hilo.

Umejazwa na kitu fulani. Huwezi kuketi pale bila kujaa kitu fulani. Una uhai fulani ndani yako. Uhai huo unakutawala, na uhai huo unatawaliwa na roho fulani.

Naam, unaweza ukajaa ulimwengu, ukiupenda ulimwengu ama mambo ya ulimwengu. Mungu na akurehemu.

Unaweza kuwa umejaa kanuni za imani kutoka kanisa fulani, maombi fulani madogo unayokariri, unafikiri kwamba ni kwenda kuomba dua kwa mtu fulani aliyekufa, ama—ama kufanya namna ya ishara juu nafsi yako. Mungu na akurehemu.

138 Nawe unaweza kuwa umejaa dini, na jambo hilo ni baya zaidi pia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Biblia ilisema, "Katika siku za mwisho wao wangekuwa wa kidini sana, wakiwa na mfano wa utauwa; wakiwa na mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake: hao nao ujiepushe nao."

Kama umejaa dini, wewe ni mwenye mashaka; dini tu, hiyo tu. Kama umejaa kanuni za imani, hujui unachozungumzia. Kama umejaa ulimwengu, wewe ni kipofu.

139 Halafu, tena, unaweza ukajaa Roho Mtakatifu. Amina. Natumaini kwamba umejaa. Na, kama hujajaa, ninatumainia utajaa. Basi kama umejaa Roho Mtakatifu, una kitu gani? Una Nguvu. Una upendo. Una amani. "Nawapa amani Yangu; siwapi kama ulimwengu unavyowapa." Una amani. Umetiwa muhuri. Una ishara. Amina. Una raha. Una furaha isiyoweza kunewa, na iliyojaa utukufu. Umetiwa nanga. Loo, jamani! Hivyo ndivyo ulivyo, ukiwa na Roho Mtakatifu. Una-. . .Kama umejaa Roho Mtakatifu, "Umepita kutoka mautini ukaingia Uzimani," ukingojea kiyama katika siku ya mwisho. Amina!

140 Katika ulimwengu ujao, katika Bwana wetu Yesu Kristo, na wale waliomwona akija katika utukufu na ukuu, "Bahari zitatoa wafu wake." "Miili ipatikanayo na mauti ya wale waliolala katika Yeye ita-. . . "

"Waliolala katika Yeye." Unaingiaje ndani Yake? "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Mwili mmoja."

"Miili ipatikanayo na mauti ya hao waliolala katika Yeye itabadilishwa na kufanywa kama ule mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, ambapo Yeye anaweza kuvitiisha vitu vyote chini Yake."

"Nikasikia sauti kutoka Mbinguni," kasema Yohana, "ikaniambia, 'Andika, "Heri wafu wafao katika Bwana. . ."'" Utaingiaje? "Kwa Roho mmoja sote tunabatizwa katika ule Mwili." [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] "'". . .wafao katika Bwana tangu sasa; wapate kupumzika baada ya taabu zao; matendo yao yafuatana nao."'" Hum!

Hilo ndilo kusudi la Yeye kumpeleka Roho Mtakatifu. Loo, dhamana yenye baraka, Yesu ni wangu! Mimi niko ndani Yake, Naye yuko ndani yangu; Baba ndani Yake, Naye ndani ya Baba; na Baba ndani yangu, nami ndani Yake.

> . . .Yesu bwangu
> Hunipa furaha ya mbingu!
> Mrithi wa wakovu wangu,
> Nimezawa kwa Roho Wake.

Amina. Singeweza kuiuza. Loo, jamani!

> Vito vyote vya dhamani na almasi, na fedha na dhahabu.
> Makasha Yake makubwa yamejaa, Yeye yuna mali isiyohesabika.
>
> Kwa maana mimi ni mwana wa Mfalme!
> Mimi ni mwana wa Mfalme!
> Nikiwa pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
> Inanifanya mimi kuwa mwana wa Mfalme!

141 Amina na amina. Singeweza kulibadilisha jambo hilo. Singeweza kulibadilisha. Nina Maandiko mawili ama matatu zaidi. . .

Halafu, hili hapa Andiko lingine. Wakati—wakati unapojazwa na Roho Mtakatifu, hayo ni mambo uliyo nayo. Basi wewe ni nini, kwa ulimwengu? Mgeni. Najua tumechelewa, bali hatuchelewi sana kwa jambo hili. [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] Mgeni! Loo!

Sisi ni wasafiri na wageni hapa,
Tunautafuta mji ujao,
Ile mashua ya uhai inakuja hivi karibuni,
Ikazikusanye johari kuzipeleka nyumbani.

142 Naweza kusikia maji yakipiga kule ng'ambo ya Mto Ohio, nilipokuwa maskini mhubiri kijana mwenye umri wa miaka ishirini na miwili, nikiuimba huo kule. Nami nikasikia, nikaangalia juu yangu, nikasikia Sauti ikasema, "Angalia juu." Hii hapa inakuja Nuru kubwa inayoning'inia kule juu, ikashuka ikaja juu yangu na kusema, "Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kule kuja kwa kwanza kwa Kristo, wewe utakuwa na Ujumbe utakaokutangulia Kuja kwa pili kwa Kristo."

Loo, ningewezaje kuamini jambo hilo? Bali lilitendeka hata hivyo. Na usiku huu mioto ya ufufuo inawaka ikizunguka-zunguka ulimwenguni. Kanisa kuu la Mungu lililokombolewa likajiinua kutoka mahali hapo, na kampeni kubwa za kuponya, na ishara, na maajabu, na miujiza, ikionyesha kule kuja.

143 Wewe ni mhamiaji, na u mgeni. Unafanya mambo ya kigeni, tofauti na uliyokuwa ukifanya. Hutendi kama ulivyokuwa ukifanya. Watu. . .Roho Mtakatifu, anapokuja juu yako, nawe unajazwa na Roho Mtakatifu, unayapuuza mambo ya ulimwengu. Unayapuuza mambo ambayo yangekuvizia. Unayapuuza. Kisha unakuwa ki—kiumbe wa kipekee, bata mwenye sura mbaya, kwao, yule tai mdogo aliyeanguliwa chini ya kiota cha kuku; niliyehubiri juu yake, *Na Hapo Tai Anapovuruga Kioto Chake*. Unaonekana kiumbe wa kuchekesha, kwao.

Lakini, loo, jamani, unatembea kwenye Barabara Kuu ya Mfalme! Amina. Loo, ni Barabara Kuu ya kwenda Mbinguni. Nami ninatembea katika Barabara Kuu ya Mfalme.

Kasema, "Mwangalie yule mtakatifu anayejifingirisha, bata yule mwenye sura mbaya. Yule ni yule mhubiri mtakatifu anayejifingirisha."

144 Mhubiri mashuhuri wa Kimethodisti alimwambia mtu fulani leo, huko Luisville, kasema, "Ningetaka kumsaidia Ndugu Billy, lakini unajua ningefanyaje? Ingenibidi kujihatarisha." Haikubidi kujihatarisha kwa ajili yangu.

Yeye aliyahatarisha Maisha Yake kwa ajili yangu. Amina! . . .?. . . Tembea tu kwenye Barabara Kuu ya Mfalme, hivyo tu. Loo, jamani! Kujazwa na Roho Mtakatifu! Kuzaliwa

na Roho Mtakatifu! Kuoshwa katika Damu Yake! Haleluya! Furaha!

145 Halafu jambo lingine, mbona, ni nini kinachokufanya ufanye jambo hilo? Ungali u mwanadamu, bali ni kitu gani kinachokufanya ulifanye? Ni kwa sababu unakuja, wewe, Roho yako inatoka juu. Ni Mungu ndani yako.

146 Nilipoenda Rumi, niliona kwamba wao, kila mmoja, alikuwa na roho ya Kirumi. Nilipoenda Uyunani, wote walikuwa na roho ya Kiyunani. Nikaenda Uingereza; wote walikuwa na roho ya Kiingereza. Unapoenda mahali mbalimbali, unaona . . . Kisha unapata roho ya Kimarekani; ni mbaya sana.

147 Nilipoingia kwenye yale mapango ya kuzikia ya San Angelo huko Rumi, walikuwa na ubao kule juu, "Tafadhalini, enyi wanawake wa Kimarekani, vaeni nguo mpate kuwaheshimu wafu." Roho ya Kimarekani.

Waangalie wakitoka kwenye ndege, wamevalia hizo nguo fupi, na kila mtu akiwaangalia, na huyu hapa anakuja Bibi Marekani. Hiyo ni roho ya Kimarekani. Unaweza kujua anakotoka; Amevaa kwelikweli, jamani, akimvuruta nyuma yake mbwa mdogo mwenye manyoya mengi na mapua yaliyojaa makamasi. Hiyo ni kweli. Loo, naam, Yeye ni . . . Yeye, yeye ni Marekani, Bibi Marekani; anashuka anaenda, mwajua, mwendo wa maringo namna hiyo. Kwa nini? Ana roho ya Kimarekani! [Ndugu Branham anapiga mimbara mara sita—Mh.] Lakini Yesu alisema, Yeye alishuhudia dhidi ya jambo hilo siku hiyo, akasema, "Ninyi mmetoka katika dunia hii chini. Mimi nimetoka Juu."

Basi kama wewe una Roho wa Kristo ndani yako, umetoka Juu, basi wewe ni mgeni hapa.

148 Lakini una tabia ya mahali unakotoka. Hivyo ndivyo ninavyojaribu kusema. Mrumi anakuja hapa, na kukuna kichwa chake; na Mjerumani anakuja hapa; Mwamerika anaenda kule. Kwa nini? Una roho ya nchi hizo unakotoka.

Jambo hilo ndilo linalotufanya tuwe tofauti sana kwa ulimwengu. Umetoka huko Juu. Umezaliwa. Wewe ni—wewe ni mwenyeji wa Ufalme mwingine. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo, ni kukufanya mwenyeji wa Ufalme wa Mungu.

149 Basi, kama wewe ni mwenyeji wa Ufalme wa Mungu, inakufanya utende namna gani? Kama Mungu afanyavyo katika Ufalme Wake. Naam, Mungu anafanya nini katika Ufalme Wake? Ni utakatifu, haki, usafi wa mawazo, usafi wa nia; Nguvu na upendo, kwenda kwa waliopotea, kuwaponya wagonjwa, kufanya miujiza, kufanya mambo makuu. Halafu, kwa ulimwengu unaonekana mwenye kichaa; nao wanasema, "Hao jamaa wamerukwa na akili zao." Mnaona? Bali wewe ni mwenyeji wa ule Ufalme.

150 Andiko moja zaidi, kama unataka kuliandika, Yohana 12:24. Hebu niwanukuulie upesi sana. Yesu alisema:

> "Kama *chembe ya ngano ikianguka ardhini*... isipokufa, haiwezi kuleta uhai mwingine."

Sasa, angalia, tamshi moja la kumalizia sasa. Pia kumbukeni, basi, ni jambo la lazima kabisa...Sasa, kwenu watu, ni jambo muhimu na la lazima kabisa, na la kushurutisha na kulazimisha, kwamba umpokee Roho Mtakatifu sasa. Kwa maana, kama usipompokea, hutafufuliwa. Sasa angalia. Mungu hawezi kuvunja sheria Zake. Tunajua jambo hilo. Yeye hufuata sheria Zake.

151 Basi, che—chembe ya ngano, ama chembe ya mhindi, tutachukua, kama Yesu alivyosema pale. Bila shaka, che—chembe, katika Biblia, ndiyo kwanza nisome jambo hilo leo, inamaanisha kitani ama namna yo yote ya mbegu, lakini, ngano, shayiri, mahindi, ama cho chote kile, ni chembe. Bali wakati chembe ya ngano inapoanguka ardhini, sasa, kuna-... Sisi sote hapa tumeona, tunajua jambo hili hutukia. Chembe ya ngano, ama chembe ya mahindi, inaweza kuonekana kamilifu iwezavyo kuwa, nawe uitie ardhini, na kama chembe hiyo...

Ina uhai unaoendelea kwa muda mrefu. Itashuka chini leo, itajitokeze katika ubua; kisha irudi chini, na kuinuka tena; na kurudi chini tena. Ni uhai unaoendelea kwa muda mrefu.

Kama chembe hiyo haina chembechembe ya uhai ndani yake, hata ionekane nzuri jinsi gani, haitainuka kamwe. Itaingia ardhini na kuoza, na ni hivyo tu. Sehemu yake, kitu chenyewe, kinaweza kutumiwa kutia mbolea na kadhalika ardhini. Bali kuhusu kuishi tena, haitaishi kamwe isipokuwa iwe na maisha yanayoendelea ndani yake. Mtu ye yote anajua jambo hilo. Huwezi kamwe.

152 Kunaweza kuwako na watu wawili, mmoja wao hasa, wote wawili wanafanana kabisa. Mmoja wao anaweza kuwa mtu mzuri, anaweza akafanya kazi nzuri, anaweza kufanya kadhalika; bali isipokuwa mtu huyo awe na Uzima wa Milele ndani yake, yeye hatafufuka kamwe katika ule ufufuo. Hawezi kufufuka; hakuna kitu mle cha kufufuka. Hakuna kitu cha kumfufua, hamna Uhai. Kwa hiyo, unaona, ndugu yangu mpendwa, dada yangu mpendwa, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kamwe kurudi kwenye Ufalme huu. Hawezi. "Hii Chembe ya ngano isipoanguka ardhini ikafa." Yeye alikuwa ananena juu ya Nafsi Yake. Bali Yeye alikuwa, si na uhai unaoendelea, alikuwa na Uzima wa Milele; na huo Uzima alikupa wewe, ili kwamba uweze kuwa na Uzima wa namna ile ile.

153 Naam, kama una uhai wa mwanadamu tu, wa kutosha kukupeleka kila mahali na kutamani. "Mwanamke aishiye katika anasa amekufa angali hai," huwezi kufufuka. Unaweza

kuwa msichana anayependwa na watu sana shuleni. Unaweza kuwa msichana anayependwa na watu sana kwenye mchezo wa karata katika shirika lenu. Unaweza kuwa mwanamke aliyevalia vizuri sana nchini. Unaweza kuwa aliye na sura nzuri sana. Unaweza kuwa aliyeumbika sana. Unaweza ukawa kipenzi kwa mumeo. Unaweza ukawa mambo haya yote, ambayo, ni vizuri sana. Lakini dada, isipokuwa una Roho Mtakatifu ndani yako, ambaye ni Uzima wa Milele, mwishoni mwa safari hii umekwisha.

Nami sijali unavyoonekana wala jinsi mambo haya yalivyo, ama jinsi unavyochukiwa na watu ama unavyopendwa nao, jinsi ulivyo mrembo ama mwenye sura mbaya; kama una Uzima wa Milele, huko utaishi milele na milele.

154 Wakati mwezi na nyote zimeondoka, na dunia imekimbia milimani na jangwani, na kila kitu kime—kime-, kimekwisha; na dunia inayombayumba kama mlevi akija nyumbani usiku, na nyote zikatae kutoa nuru, na zianguke kutoka mbinguni, na mwezi ugeuke kuwa damu; na ju—jua litahayari na kuuficha uso wake, watakapomwona Mwana wa Adamu akija. Utang'aa katika haki ya Yesu Kristo, upate kutoka kaburini kama kijana mwanamke mrembo, kuchukua mwenzio, mkaishi milele na milele na milele, na nyakati zote za Milele utakuwa ungali unaishi bado. Hilo ndilo kusudi la Roho Mtakatifu.

Kama ukisikia mvuto ulio mdogo sana, usimkatae.

155 Roho Mtakatifu ni nini? Mungu ndani yako. Ni wa ajili gani? Kuendeleza kazi miongoni mwa watu Wake; kulikusanya Kanisa Lake pamoja, kulileta Kanisa kufikia mahali katika siku hii, juu zaidi ya Kiluteri, Kimethodisti, na Kipentekoste, kufikia mahali pa kufanywa wana mwenye mamlaka na neema ya Kunyakuliwa. Ili kwamba, wakati sehemu ya Kanisa, wakati Roho atakapoingia kwenye Kanisa hili hapa, litafufuka tu; nalo litawaleta, litawaleta wote waliokombolewa ambao wamemgusa Roho yule.

Waluteri hao waliosimama pale pamoja na nuru yote waliyokuwa nayo, katika kuhesabiwa haki; Wamethodisti hao walioanguka sakafuni, kisha wao wakawamwagia maji usoni, mwao—kutokana na kuguswa kwao na Roho kupitia kutakaswa; Wapentekoste hao, ambao walitembea huku na huko mitaani nao wakawaita "vilugha, na watatarikaji, na lugha ya baradhuli," na yote hayo; wao watasimama katika haki, mbele za Mungu kwenye Siku ile, hakika tu kama vile Biblia hii inavyosimama hapa. Kama mnaniamini mimi kuwa mtumishi. . . Mnaniita nabii Wake; mimi sijiiti hivyo. Lakini, sikilizeni, mimi ninawaambia katika Jina la Bwana. Hao walio katika Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye katika kule kuja Kwake, kwenye ule ufufuo, na ni wale walio katika Kristo.

Tunaingiaje katika Kristo, jamani?

156 Kwa kanuni moja ya imani sote tunajiunga mle? La. Kwa kupeana mkono mara moja sote tunavutwa ndani? La. Kwa maji moja sisi sote tunabatizwa mle? La. Ama kwa madhehebu moja sisi sote tunaingizwa kwenye madhehebu? La.

"Lakini, kwa Wakorintho wa Kwanza 12:13, "Kwa Roho mmoja, Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, sisi sote..." Methodisti, Batisti, Mluteri, Mpresbiteri, "Tukienenda Nuruni, kama Yeye alivyo katika Nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na Damu Yake Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yatusafisha udhalimu wote." Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, nasi tumefanywa washiriki wa neema Yake."

157 Huwezi kwenda Hukumuni. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini." Hakuna mtu awezaye kuamini mpaka awe na Roho Mtakatifu. "Na kumwamini Yeye aliyenipeleka," wakati Roho Mtakatifu ameshuhudia juu ya kufufuka Kwake. "Yuna Uzima wa Milele, naye hataingia hukumuni kamwe, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ati nini? Hutapatikana na Hukumu kamwe. Hutasimama kamwe kwenye kile Kiti Cheupe cha Enzi ukahukumiwe.

Unakabiliana na hukumu yako papa hapa. Umejihukumu unapohukumu na kusema, "Mimi sifai, na elimu yangu haifai kitu. Bwana, njoo ndani yangu, ukanichukue na kuniongoza, Bwana. Sijali unavyosema ulimwengu huu wenye kichaa. Niongoze, Bwana, kwa Roho Wako." Umetoa hukumu wakati huo. Ukajihukumu kama mpumbavu kwa ajili ya Kristo, na, katika haki Yake, Siku ile tutasimama wasiopatikana na mauti katika mfano Wake.

158 Ni njia moja tu. Vipi? "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Basi unapokuwa katika Mwili huo, hukumu tayari imeuhukumu Mwili huo, nawe umemkubali kama kipatanisho cha dhambi zako.

Unasema, "Nimefanya jambo hilo, Ndugu Branham."

Basi, kama Roho Mtakatifu amerudi akakupa muhuri kama ishara, Roho huyo anakuleta katika Mwili wa Kristo. Unageuka upande ule mwingine, nawe ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu. "Umepita kutoka mautini ukaingia Uzimani. Mambo ya kale yamepita, nawe ni mpya katika Kristo!" Amina!

159 Loo! Tafadhali, hebu nikushawishi, ndugu yangu Mkristo ama dada. Usiache ufufuo huu ukupite. Huna budi kumpokea Roho Mtakatifu. Ni nini? Roho wa Mungu. Alikua kwa ajili gani? Kukuongoza, kukuelekeza, kukujaza, kukutakasa, kukuita utoke, uingie katika lile Kanisa.

Kanisa ni nini? Neno *kanisa* lina maana gani? "Walioitwa watoke, waliotengwa." Loo, jinsi ningeweza kuchukua mahubiri kutoka kwa jambo hilo sasa hivi! "Walioitwa watoke, waliotengwa," wageni, mbali na ulimwengu, wasafiri na wageni,

tukikiri ya kwamba hatuna mji hapa wa duniani ambao tunatamani kuishi ndani yake. Loo, jamani!

160 Kama Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, walivyokaa, wakiishi katika hema nchini. Wao walikiri walikuwa wasafiri na wageni, mzao wa mrithi, mrithi kule nyuma; baba, mrithi. Sisi ni mzao wao. "Nao walikuwa wakiutafuta Mji ambao Mwenye Kuujenga na Mwenye Kuutengeneza ni Mungu." Amina. Wao walikuwa wakitafuta.

161 Na leo mzao wao angali anautafuta Mji unaokuja, akisema, "Sitaki kujizoeza ulimwengu huu. Sitaki uhusiano wo wote na ulimwengu huu. Nataka, ninautafuta Mji ambao umejengwa mraba. Ninautafuta Mji ambao una Uzima wa Milele, ambamo jua halitatua kamwe, ambamo hakutakuwepo na uzee, ambamo hakutakuwa na dalili ya mfiwa kwenye kifundo cha mlango, wala kaburi chini ya kilima. Ninautafuta Mji, ambao Mwenye Kuubuni na Kuujenga, wa Mungu."

162 Kuna njia moja tu ya kuupata. "Kulikuwa na Jiwe lililochongwa mlimani, bila kazi ya mikono, ambalo lilifingirika ulimwenguni na kuupondaponda, nao ukawa kama ngano... ama makapi katika sakafu za kupuria." Hebu Jiwe hilo, yule Yesu Kristo; Jiwe hilo la kujikwaa kwa ulimwengu, Jiwe la kuchukiza, Jiwe la kuchekelewa, Jiwe la kujikwaa kwa kanisa; bali Jiwe lenye thamani na Sumaku kwa mwamini, Jiwe la dhamana, Jiwe la raha. Loo, Jamani!

Raha! Ninajua ya kwamba nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Nafsi yangu iko katika raha. Loo! "Njoni Kwangu ninyi msumbukao na wenye kulemewa na mizigo mizito, nami nitawapa raha ya nafsi zenu." "I—Ishara ambayo itanenwa mabaya," kasema yule na—nabii kwa Mariamu. Itakuwa ni Ishara, hakika, itakuwa. Bali itakuwa ni dhamana. Itakuwa upendo. Itakuwa ridhaa. Itakuwa ni kitu ambacho unachojua umepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

163 Ndugu yangu, dada yangu; kama ndugu yenu, kama mtumishi wenu katika Kristo, hebu nikushawishi, kwa moyo wangu wote. Usiache jambo hili lipite juu ya kichwa chako, ama lipitie karibu nawe, wala chini yako. Mpokee moyoni mwako, nawe utakuwa mtu mwenye furaha duniani.

Sikuahidi utapata dola milioni moja. La, bwana! Ndugu Leo, nafikiri kuna mengi sana ya hayo yameahidiwa sasa, "mamilioni ya dola," mambo ambayo watu mbalimbali walisema. "Kama ungekuwa Mkristo, ungepata dola milioni moja, nawe utakuwa tajiri." Mimi siwaahidi kitu.

Ninawaahidi kitu hiki, kitu pekee ninachoweza kuwaahidi, wokovu Wake. Neema yake imetosha kwa ajili ya kila jaribu. Wale watu kwenye Pentekoste, hata hawakutaka waliyokuwa nayo. Ati sasa mnene kuhusu mamilionea? Wao hawakutaka waliyokuwa nayo, Dada Angie.

164 Ningetaka kukusikia wewe na Gertie mkiimba, moja ya siku hizi, (yuko wapi?), *Juma la Kurudi Nyumbani*, moja ya siku hizi. Wengi wao tayari wamepita mpakani tangu wakati huo. Loo, jamani!

Wao hawakuomba mambo makuu. Hawakuomba pesa. Mbona, Petro alisema, "Fedha na dhahabu sina, bali nilicho nacho, nitakupa wewe."

Nami ninasema jambo hilo usiku huu, marafiki. Furaha, upendo, dhamana, niliyo nayo ya Kristo na kufufuka Kwake, nilicho nacho, ninawapa ninyi; ninawapa ninyi, kama wana wa Mungu.

Nawe njoo ukae msalabani iwapo Mungu alikuita, wala usisimame. Mtakapokuja kesho usiku, njoni aidha mwingie hapa na kukaa hata jambo hilo litakapomalizika; ama mje, nasi tutawaombea na kuwawekelea mikono. Nendeni . . . Hiyo ndiyo taratibu ya Biblia, kuwawekelea mikono kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Kisha tutaenda, mtaenda nyumbani kwanu . . . Kama ukikaa pale pale, kama ukikaa usiku kucha, ukae kesho yake, na ukae siku inayofuata, ukae likizo yote, ukae mpaka mwanzoni mwa mwaka, na kuendelea kukaa, kaa hata.

165 Hilo, lo lote tutakalowashauri juu ya kesho usiku, tukiwaonyesha ninyi katika Biblia kile hakina budi kutukia, kitatukia. Basi hapo atakapokuja Yeye, basi hamna pepo wa kutosha matesoni . . . Unajua umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. U kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Kengele za shangwe za Mbinguni zitalia.

166 Ndugu Othal, ninakwambia, jambo hilo linakutia tu moto. Huyu hapa maskini mvulana anayeketi hapa, maskini ndugu yangu, aliyekuwa jambazi lililotembea huku limebeba bunduki umbavuni mwake, limtafute mtu pembeni, mtu fulani apate kuwaua kinyama. Basi nini kilitukia? Siku moja aliangalia na akaamini akapata Uzima. Naye akaendelea mbele. Akaifuata mikutano yangu. Basi maskini jamaa huyo, bila chakula cha kutosha, huku analala kwenye vijiti kando ya hema, akiona njaa na kiu. Ndipo siku moja Roho Mtakatifu akaja. Loo, Ndugu yangu, jambo hilo lilikubadilisha, sivyo? Lilileta Uzima na kuondoa mauti. Chuki ikaondoka, upendo ukaingia. Loo, jamani! Uadui na kuzozana kwote kukaisha; Maisha mapya yakaingia.

Angali hapa kwa wengine mara wengine, wengine mara wengine, na kila mahali kule. Loo, kengele za shangwe za Mbinguni zikilia! Enyi marafiki, hakuna njia kwangu ya kulielezea jambo hilo.

167 Sikilizeni, ili kwamba nipate kuacha jambo hili, kama mmeamini ushuhuda wangu, kama mtumishi wa Kristo, na nimejaribu kuwaonyesha kutoka kwenye Biblia ya Mungu ni kweli. Na iwapo maneno yangu yanaonekana kana kwamba

huenda yakawa kidogo mageni juu ya jambo hili, angalieni ile picha katika ulimwengu wa kisayansi. Angalieni matunda, ambayo Nguzo hii ya Moto iliyowangoza wana wa Israeli, angalieni matunda inayozaa. Angalieni kile ifanyacho, kile isemacho.

Si mimi ninayenena; ni Yeye anayenena kupitia kwenu, mnaona. Si mimi ninayeona maono; ni Yeye anayenena kupitia kwenu. Si mimi ninayewaponya wagonjwa; ni Yeye aliye ndani yenu, anayewaponya wagonjwa. Si mimi ninayehubiri; mimi ni mwoga wa nyuma, ambaye analikimbia hilo wazo, bali ni Yeye anayenena waziwazi. Mimi silijui Neno; bali Yeye analijua. Ndivyo ilivyo. Ndivyo ilivyo. Hivyo ndivyo ilivyo.

Ndiye Yule pale. Basi Malaika yuyo huyo wa Mungu yuko papa hapa kwenye jengo hili usiku wa leo. [Ndugu Branham anagonga mimbara—Mh.] Loo, jinsi ninavyompenda!

168 Sasa ni wangapi wanaotaka kumpokea Roho Mtakatifu? Tuyachunguze maisha yetu. Ni wangapi hawajampokea, nao wanataka kumpokea? Inua mkono wako juu, useme, "Ndugu Branham, vilindi vya moyo wangu, nataka kumpokea Roho Mtakatifu." Mungu awabariki, kila mahali.

169 Ni wangapi wenu ambao mmempokea Yeye, na wangetaka kwenda kama walivyofanya katika Matendo 4 na kusema, "Ee Bwana, Ee Bwana, nyosha mkono Wako kuponya, na konyesha ishara na maajabu katika Jina la Mwana Wako Mtakatifu Yesu, na unipe ujasiri wote na upendo kunena, na kujazwa kupya"? Naam, huu wangu, pia. Mungu na anipe.

Na tuinamishe vichwa vyetu, katika uaminifu kabisa, kila mtu akishikilia shauku yake moyoni mwako.

170 Bwana Yesu, tunafunga kusanyiko hili ndogo usiku huu, baada ya kushiriki kwenye Neno na Roho Mtakatifu. Jinsi amekwisha tubariki na kumwaga mioyoni mwetu mafuta ya Neno Lake! Kuna wahudumu, kuna watu hapa ambao walikuwa kila tabaka ya maisha, ambao wameonja na kuona Bwana ni mwema. Tunajua Roho Mtakatifu ni nini sasa, ahadi ya Mungu. Ni Uzima wa Milele kwa wote wanaoamini.

171 Nasi tunajua ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa ni Roho wa Yesu Kristo aliyerudishwa, Naye yumo ndani yetu leo. Kama Mungu alivyokuwa juu yetu, katika Nguzo ile ya Moto; kisha akatembea pamoja nasi katika mwi- . . . mwili ulioitwa *Imanueli*, "Mungu pamoja nasi"; na sasa Yeye yumo ndani yetu, kwa Roho Mtakatifu, Mungu ndani yetu. Loo!

Yesu alisema, "Siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba Yangu, nanyi ndani Yangu, Nami ndani yenu. Mtafahamu jambo hilo siku hiyo. Kwa maana, mko katika ulimwengu wenye giza, kama tusemavyo, sasa, lakini siku hiyo mtafahamu."

172 Baba, lisingeweza kufanywa dhahiri sana na kamilifu, kwa maana basi tusingekuwa na kitu cha kuwa na imani kwa ajili yake. Lakini kazi zote za Mungu zinatawalwa na imani. Na kwa imani katika Neno Lako, kwenye ushuhuda wa Roho Mtakatifu ambaye tunajua yuko sasa, naomba kwamba kila mtu mwenye njaa hapa atajazwa na Roho Mtakatifu. Wale wasiye Naye, na wanaona njaa kwa ajili Yake, kumbukeni tu . . . Tungewaambia, Bwana, kama jambo hili ulilosema Wewe, "Heri ninyi mnapoona njaa na kiu. Mtashibishwa." Hiyo ni ahadi. Na hata ni baraka kuwa na njaa. Umebarikiwa hata kujua ya kwamba Mungu amenena nawe, kwa maana Yeye alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza."

173 Basi, Bwana, hao walio mashujaa wa zamani hapa, wameinua mikono yao. Nilikuwa nimeinua wangu. Ee Bwana, tupe nguvu, tupe Nguvu kunyosha mkono wa Mtoto Wako mtakatifu Yesu, ili kwamba ishara na maajabu zifanywe, ili ipate kuwa huduma yenye kilindi, jambo kubwa kuliko lililopata kutokea bado. Tupe ujasiri na upendo, kunena na watu. Tujalie, Bwana. Kuwa pamoja nasi katika mambo yote, tunaomba katika Jina la Yesu.

174 Basi kesho usiku, Bwana, na kuje upepo wa nguvu sana ukienda kasi, ushuke kwenye jengo hili, hata itakuwa tu kama Siku nyingine ya Pentekoste. Msingi umekwisha wekwa. Kila kitu kiko tayari. Maksai wamechinjwa, ndama walionona wamechinjwa, kondoo dume wamechinjwa; meza imeandaliwa, wageni wamealikwa. Ee Bwana, tuma sikukuu ya Pentekoste, kesho usiku, kwenye jengo hili, na kumjaza kila mtu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tujalie, Baba. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

> . . . tunajifunza mambo mengi,
> Tutakuwa na kinubi cha dhahabu, labda nyuzi elfu moja;
> Tutaimba na kupiga makelele na kucheza kila mahali, Mwana-Kondoo atayafuta machozi yetu;
> Tutakuwa na kurudi nyumba- . . . juma moja la kurudi nyumbani, maika elfu kumi ya kwanza. Amina!
>
> Damu ya dhamani ya Mwana wa Mungu Mwenyewe imetusafisha na kututakasa
> Watu wa ajabu kwa ajili ya Jina Lake nao wanaitwa Bibi-Arusi
> Ingawa hapa wametupwa na wanadharauliwa, siku moja Bwana atawaleta
> Hao waliochaguliwa karibu na lango, na hilo linastahili sana.
> Tutakapokuwa ndani ya yale malango ya lulu, tutajua . . .

*Roho Mtakatifu Ni Nini?*
(*What Is The Holy Ghost?*)
16 Desemba, 1959, Jumatano jioni

*Roho Mtakatifu Alitolewa Kwa Kusudi Gani?*
(*What Was The Holy Ghost Given For?*)
17 Desemba, 1959, Alhamisi jioni

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa katika Kiingereza katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. Kila juhudi imefanywa kuzitoa jumbe hizi kwa usahihi sana kutoka kwenye kanda za sumaku na kuziandika katika kitabu, nazo zinachapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2009.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org